# Nipashe

Alhamisi Aprili 25, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579901

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Neema ajira mpya 5,400 zikitangazwa na serikali

UKURASA 3



ama

ALHAMISI APRILI 25, 2019

AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 20

Aliyezirai miaka 27 azinduka mzima

Ukurasa 16

Mashine ya kipekee Afrika nzima kutibu kansa yaletwa

Ukurasa 15

TB ilivyosimamiwa, UN inavyoagiza mwelekeo

MJUE PROFESA KAISI WA SASA

Anaambatanisha ubingwa wake hospitalini, imani kuuwezesha ujauzito ulioshindikana

Ukurasa 18

UKURASA 13

# NSSF yafunguka ulipaji wa mafao


• **Yaeleza** wenye 'nyumba ndogo' wanavyoipa tabu... *Endelea ukurasa 2*



Rais John Magufuli akiwa na mwenyeji wake, Rais wa Malawi, Prof. Arthur Peter Mutharika, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kamuzu, Lilongwe jana, kwa ziara ya kiserikali ya siku mbili. **PICHA: IKULU**

## Tahadhari kimbunga kikubwa yatolewa

UKURASA 2



## Tarehe ya kuzimwa laini za simu yatajwa

UK.2

**MICHEZO** **AUSSEMS AIANDALIA KMC KIKOSI TOFAUTI** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Tahadhari kimbunga 'Kenneth' yatolewa

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA), imetoa tahadhari kuwa Tanzania itakumbwa na kimbunga kiitwacho 'Kenneth' kinachotarajiwa kuambatana na mvua kubwa na kusababisha madhara makubwa ukiwamo uharibifu wa mali na miundombinu.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Miundombinu na Huduma za Ufundi wa TMA, Dk. Pascal Waniha, alipozungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo. Alisema kimbunga hicho hadi leo mchana kitasogea ukanda wa Tanzania takriban kilometa 150 kwa saa.

Dk. Waniha aliyataja maeneo yatakayopata madhara ya kimbunga hicho kuwa ni Lindi, Mtwara, Ruvuma na ya jirani yaliyoko takriban kilometa 500 kutoka kwenye mikoa hiyo.

Alisema kimbunga hicho kitakuwa na ukubwa wa mwendokasi unaozunguka takriban kilometa 130 kwa saa na wakati akizungumza jana kilikuwa kilometa 100 kwa saa na hadi mchana wa jana kilisogea zaidi na kufikia kilometa 450 katika ukanda wa pwani.

"Usiku wa kuamkia kesho (leo), kitafikia kilometa 250 na upepo utakuwa kilometa 150 kwa saa, kesho mchana (leo) kimbunga kitakuwa kilometa 150 kutoka katika ukanda wetu na mwendokasi wake utakuwa kilometa 150 kwa saa," alisema.

Dk. Waniha alitaja athari zitakazojitokeza kuwa ni mafuriko makubwa ambayo yataambatana na kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari na kusababisha uharibifu wa miundombinu, makazi ya watu yakiwamo mapaa kuezuliwa na uharibifu wa mazao.

"Tunaongelea kilometa 100 kwa saa ila kabla hakijafika, mwendokasi wake utakuwa kilometa 170 na kitapungua kutokana na mazingira yaliyopo," alisema.

# NSSF yafunguka ulipaji wa mafao

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umeeleza jinsi unavyolipa mafao ya wastaafu na warithi kwa mujibu wa sheria.

Vilevile, umeeleza kuwapo kwa changamoto za migogoro ya kifamilia na wenza kutengeneza nyaraka ili kujipatia fedha, huku kukiwa na uchunguzi wa kina kwa kila anayepeleka nyaraka.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe ofisini kwake jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, alisema malipo ambayo yanathibitishwa kuwa yapo kwa mujibu wa sheria yanafanyika bila ucheleweshaji.

"Mambo yanayohusu fedha yanahitaji umakini mkubwa sana, tunapopokea maombi ya mtu, tunaanza uchunguzi wetu kwa kutumia kitengo maalum, tukishajiridhisha na nyaraka pamoja na matakwa ya kisheria ndiyo malipo yanafanyika," alisema.

Alibainisha kuwa wapo wanaolalamika lakini wakifuatilia kwa kina, wanabaini kuwa hawastahili kwa kuwa bado wapo kazini, nyaraka siyo halali na wengine wana nyaraka feki au hawastahili kulipwa wao bali watu wengine.

Kwa mujibu wa Erio, kwa kipindi cha Januari hadi Machi, 2019, mafao ya wastaafu yalilipwa ni Sh. bilioni 97.031 ambayo hulipwa kila tarehe 25 ya mwezi na fao la kukosa ajira Sh. bilioni 36.55.

Alisema kwa miezi hiyo mitatu, warithi 285 walilipwa malipo ya mkupuo maalum ya Sh. bilioni 2.4, huku wategemezi wao wakilipwa fedha za kila mwezi Sh. bilioni 1.48 na kufanya jumla ya Sh. bilioni 3.88.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2018, warithi wanalipwa pensheni ya kila mwezi kwa miezi 36 baada ya mstaafu kufariki dunia.

"Eneo la warithi lina changamoto kubwa kutokana na familia husika hasa zenye migogoro kama kwa aliyekuwa na wake wengi au ndugu wanaotaka kupata fedha hizo.

"Wakati mwingine tunapata

INAENDELEA UK. 8



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza na Katibu wa Bunge la Zambia na Mwenyekiti wa Chama cha Makatibu Mezani Kanda ya Afrika, Cecilia Mbwewe (katikati) na Katibu wa Bunge la Jimbo la Free State, Afrika Kusini, , Thabo Mofokeng, walipomtembelea ofisini kwake jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**


KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DAR ES SALAAM
UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI
MIRATHI Na. 20 YA MWAKA 2019
MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI
YA MAREHEMU FERDINAND SAUDARI SWAI
MWOMBAJI/WAOMBAJI
ROSE ANDERSON SWAI
SENI SONGWE MALIMI

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 13 mwezi wa Mei 2019.

Imewasilishwa Dar es Salaam, leo tarehe 10 mwezi wa 04 2019.

…………………………………………
NAIBU MSAJILI
NAKALA KWA:
…………………………………………
…………………………………………
…………………………………………

NAIBU MSAJILI

115194002


# Serikali kuzima laini za simu Desemba 31

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imepanga kuzima laini zote za simu za mkononi nchini ambazo zitakuwa hazijasajiliwa kwa alama za vidole ifikapo Desemba 31, mwaka huu.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, alisema bungeni jijini Dodoma jana kuwa usajili huo ambao umepangwa kuanza Mei Mosi, mwaka huu, utailazimu serikali kufanya mapitio yake Septemba mwaka huu. "Kwa mujibu wa takwimu tulizonazo kama Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kupitia kwa Nida (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa), watu ambao wana namba za vitambulisho vya taifa wapo milioni 16.

"Hata hivyo, hili zoezi litaanza tarehe 1 Mei, 2019 na tutafanya 'review' (mapitio) mwezi wa tisa (Septemba) ili kuona ni watu wangapi wamekwishasajiliwa na kuna changamoto kiasi gani, lakini mwisho kabisa wa zoezi hili itakuwa tarehe 31, Desemba 2019 ambapo tutazima laini zote za ambao watakuwa hawajajisajili kwa kutumia alama za vidole," Nditiye alisema.

Naibu waziri huyo alikuwa akitoa ufafanuzi kuhusu mwongozo ulioombwa na Mbunge wa Viti Maalum, Felista Bura (CCM), aliyetaka majibu ya serikali kuhusu malalamiko ya wananchi wengi ambao hawajapata vitambulisho hivyo, huku wakiwa na wasiwasi kwamba inawezekana laini zao zikafungwa kutokana na kutopata vitambulisho vya taifa.

Nditiye alisema kuanzia Mei Mosi, mwaka huu, kampuni zote za simu zitatakiwa kusajili laini za simu kwa kutumia alama za vidole, baada ya kujiridhisha na utambuzi wa mtu kupitia kitambulisho cha taifa. "Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi tumezichukua kwa muda mrefu kuanzia Machi tulipozindua rasmi usajili kwa kutumia alama za vidole kwa mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza kwa majaribio na sasa hivi ndiyo tunataka kuanza tulifanye kama rasmi baada ya kujiridhisha kwamba taratibu zote ziko sawa sawa," alisema.

Hata hivyo, kauli hiyo ilimwinua kitini, Mwenyekiti wa Bunge, Andrew Chenge, akisema katika tangazo lililotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kusajiliwa wanataka uwe na kitambulisho cha taifa, na hiyo ndiyo hoja inatakiwa kufafanuliwa vizuri maana maeneo mengi wananchi wengi hawajafikiwa na vitambulisho hivyo. Chenge alimtaka Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola kutoa ufafanuzi zaidi ili wananchi wasiwe na maisha ya wasiwasi na lazima waendelee kutumia simu zao. "Mheshimiwa Mwenyekiti, Nida tulikuwa na lengo la kutambua na kutoa vitambulisho milioni 24.5, hayo ndiyo malengo, lakini mpaka sasa, Nida tumekwishafanya utambuzi, usajili wa watanzania wenye sifa milioni 16.

"Tulipoona kwamba wenzetu wa TCRA wanataka kubadilisha masuala ya kusajili simu ili waweze kutumia alama za vidole na kwamba mwenye kitambulisho cha taifa ndiye atakayesajiliwa, sisi kupitia Nida tuliweka utaratibu.

"Watanzania ambao wamekwishapata vitambulisho, watawasilisha vitambulisho vyao. Watanzania milioni 16 tayari wameshapatiwa namba inaitwa NIN yaani National Identification Number. Kwa hiyo, namba hiyo ambayo anasubiri apewe kitambulisho chake, ndiyo atakayoiwasilisha TCRA, atabofya kidole chake pale namba hiyo na atasajiliwa," Lugola alisema.

## HABARI KITAIFA

# Neema ajira 5,000 serikalini

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

SERIKALI imetangaza kutoa ajira 5,410 kwa Jeshi la Polisi, Magereza, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Akiwasilisha jana bungeni jijini Dodoma hotuba ya makadirio bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alisema lengo kuwapo kwa ajira hizo ni kuimarisha usalama nchini.

Lugola alisema ajira hizo zitakwenda sambamba na kuwapandisha vyeo maofisa, wakaguzi na askari na kutoa mafunzo ya kitaaluma na kimedani ndani na nje ya nchi. Alisema wizara yake itaimarisha upekuzi wa askari na vijana wanaoomba kujiunga kwenye majeshi hayo ili kuwa na askari wenye nidhamu na moyo wa kulitumikia taifa.

"Katika mwaka 2018/19, Jeshi la Polisi limeajiri askari wapya 812 kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kazi za polisi. Askari hao wamehitimu mafunzo ya awali katika Shule ya Polisi (MPA), Aprili 9, mwaka huu," alisema.

Alibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya askari 3,725 wanatarajiwa kuajiriwa kupitia Jeshi la Polisi huku akibainisha kuwa maofisa na askari 55 wanashiriki operesheni za ulinzi wa amani katika nchi mbalimbali zikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Sudan, Sudan Kusini, Ethiopia na Lesotho.

Alisema wizara hiyo inaomba kuidhinishiwa na Bunge Sh. bilioni 921. 247 kwa ajili ya bajeti yake kwa mwaka ujao wa fedha.

**MAUAJI YA WATOTO NA VIKONGWE**

Kuhusu mauaji ya watoto na vikongwe, waziri huyo alisema miezi ya Novemba na Desemba mwaka jana, yaliibuka matukio ya mauaji na utekaji watoto kwenye mikoa ya Njombe na Simiyu.

"Matukio hayo ni uhalifu mpya kutokea katika mikoa hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2012. Katika mikoa ya Njombe, watoto sita waliuawa na watatu walitekwa ambapo polisi walifanikiwa kuwapata watoto waliotekwa wakiwa hai. Kutokana na matukio hayo, watuhimiwa saba walikamatwa na kufikishwa mahakamani kwa hatua za kisheria," alisema.

Alisema KUWA katika Mkoa wa Simiyu kulitokea mauaji ya watoto wanne ambao waliuawa na kukatwa baadhi ya viungo. Alisema watuhumiwa 12 walikamatwa na kufikishwa mahakamani kutokana na matukio hayo.

Waziri huyo alisema polisi wamefanikiwa kudhibiti mauaji ya vikongwe kutoka 117 yaliyoripotiwa mwaka 2017/18 hadi matukio 57 kwa mwaka huu wa fedha.

"Hali inaonyesha mauaji ya vikongwe yamepungua kwa asilimia 51.3. Matukio hayo yalijitokeza kwenye mikoa ya Geita (7), Iringa (1), Kigoma (2), Lindi (1), Mbeya (3), Mwanza (6), Njombe (3), Rukwa (2), Ruvuma (2), Shinyanga (3), Simiyu (4), Songwe (7) na Tabora (16).

# Mariam ahamishiwa Ocean Road

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya timu ya madaktari wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kukutana kujadili ripoti ya uchunguzi wa Mariam Rajab (25), mkazi wa Kitongoji cha Inung'una mkoani Singida mwenye kidonda sugu mgongoni, imekubaliana mgonjwa huyo ahamishiwe leo Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa matibabu.

Daktari Bingwa Mkuu wa Idara ya Upasuaji hospitali ya Muhimbili, Dk. Ibrahim Mkoma, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa Mariam anatarajia kuhamishiwa leo taasisi ya Ocean Road.

Dk. Mkoma alisema baada ya majibu ya vipimo mbalimbali walivyomfanyia mgonjwa huyo kutokana na jana kuvijadili, wameshauri ahamishiwe Taasisi ya Ocean Road kwa ajili ya kupatiwa matibabu zaidi.

Mariam amefanyiwa vipimo vya CT-scan ya kifua na kichwa, Ultrasound pamoja na vipimo vingine mbalimbali vya damu ambavyo vimesaidia kubaini ugonjwa unaomsumbua.

"Kama mnavyojua majibu ni siri baina ya daktari na mgonjwa hivyo tunamuhamisha kutoka hospitali Muhimbili kwenda Ocean Road kwa sababu taasisi za serikali zimegawanywa na kila moja imepewa uwezo wake ndio maana tumeona aende huko kwa ajili ya kuendelea na huduma ya matibabu," alisema.

Mariam alipokelewa hospitalini hapo mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya kuonekana mtandaoni akiomba msaada wa kufikishwa hospitali ya Muhimbili kwa matibabu kutokana na familia yake kuwa maskini.

Akizungumza na waandishi wa habari, Dk. Mkoma alisema Mariam ataanza matibabu rasmi katika taasisi hiyo na atakapomaliza atarejeshwa Muhimbili kuendelea matibabu mengine.

"Tunamuhamishia Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kwa sababu zipo baadhi ya huduma za matibabu ambazo anapaswa kupatiwa kutokana na ugonjwa unaomsumbua," alisema.

Naye, Mariam alieleza kufurahishwa na huduma alizopatia tangu apokelewe hospitali ya Muhimbili ambazo zimemuwezesha kutembea vizuri.

"Hivi sasa naendelea vizuri, tangu nimekuja Muhimbili naendelea vizuri. Kabla sijafika hapa nilikuwa siwezi kutembea vizuri lakini sasa naweza kutembea vizuri," alisema.

Takribani wiki mbili zilizopita, Mariam ambaye alipokelewa hospitali ya Muhimbili alilazwa wodi namba 15 jengo la Kibasila, alisimulia namna ambavyo ameteseka na kidonda hicho ambacho chanzo chake ni moto.

CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz @capitalradiotz

WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI (RITA)

TAARIFA KWA UMMA

UTARATIBU WA KUHAKIKI VYETI VYA KUZALIWA NA VIFO KWA WAOMBAJI WA MIKOPO YA ELIMU YA JUU KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) umeanza Uhakiki wa Vyeti vya Kuzaliwa na vyeti vya vifo (ikiwa muombaji amepoteza mzazi mmoja au wote) vya waombaji wanaotarajiwa kuomba mikopo ya masomo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mwaka 2019/2020. **Maombi yote yatafanyika kwa njia ya mtandao pekee**.

Waombaji wanaohakiki wanatakiwa kufuata maelezo yafuatayo:

1- Kila muombaji aingie katika mtandao kwa anuani: ***http://uhakiki.rita.go.tz/uhakiki/*** ili kujisajili na kupata akaunti maalumu ambayo atatumia kutuma nakala ya cheti kinachohakikiwa, namba ya uthibitisho wa malipo/ risiti (*ambayo atatumiwa kwa ujumbe wa simu malipo yanapokamilika*) na kupokea nakala ya cheti kilichohakikiwa.

2- Ada ya uhakiki kwa kila cheti ni TShs. 3,000/= (elfu tatu) ambayo italipwa kwa njia mojawapo kati ya zifuatazo:

- Kupitia Benki au Mawakala wa Benki ya NMB au CRDB kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (*control number*) **991380913455.**
- Kulipia kwa Simu kupitia M Pesa, Tigopesa, T Pesa, Airtelmoney au Halopesa kwa namba ya kampuni **001001** na kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (*control number*) **991380913455.**

Malipo yatakuwa yamekamilika baada ya muombaji kupokea risiti kwa njia ya ujumbe wa simu kutoka namba **15200** kupitia namba aliyotumia kufanya malipo au namba aliyoulizwa na mhudumu wa benki/ wakala.

**MUHIMU:**

- Kila muombaji afungue akaunti binafsi ya uhakiki na atunze nywila( *password*) ya akaunti yake.
- Tuma kivuli cha cheti kinachosomeka vizuri na hakikisha namba ya ingizo (*entry number*) inasomeka vizuri.
- Utapokea ujumbe wa kukiri kupokea nyaraka zako kwa maombi yaliyotumwa kikamilifu.
- Majibu ya uhakiki yatatumwa katika akaunti uliyofungua.

**Kwa maswali na maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia:**
**Simu:** 0800117482 (*bila malipo*) / **Barua pepe:** ***info@rita.go.tz***

Emmy Kalomba Hudson
**Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu/ Afisa Mtendaji Mkuu – RITA**

215192502

April 23, 2019

# MCT yadai uhuru wa wananchi kupata habari

**Na Beatrice Moses**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limeeleza kuwa watetezi wa uhuru wa vyombo vya habari wanalenga katika kulinda haki ya wananchi kuwa na uhuru wa kupata habari mbalimbali zikiwamo za kuwaletea maendeleo.

Akizungumza jana kwenye hafla ya uzinduzi wa vitabu vitatu vinavyohusu taaluma ya habari Mwenyekiti wa Kamati ya MCT ya Maadili, Jaji mstaafu Juxon Mlay, aliyekuwa mgeni rasmi alieleza umuhimu wa uhuru wa vyombo vya habari.

"Tunalinda au tunaweza kutetea uhuru wa vyombo vya habari kwa sababu ni msingi wa uhuru wa wananchi kupata habari siyo kwa sababu sisi tuna haki ya kuwa na uhuru," alisema.

Jaji Mlay aliwataka waandishi wa habari kuongeza umakini katika matumizi ya lugha kwa kuhakikisha wanatumia lugha fasaha ili kulinda soko la wasomaji na wasikilizaji, kwa kuwa makosa kama hayo yanaweza kusababisha chombo husika kubezwa. "Makosa ya kiuandishi yanakera wasomaji au wasilikilizaji yanaweza kumkimbiza, mfano kukinukisha! lina maana gani , ni vyema kutumia lugha fasaha ili kuikuza lugha yetu," alisema. Alisema katika hafla hiyo pamoja na mambo mengi yameelezwa, hata hivyo kuna angalizo la kuanguka kwa utamaduni wa wananchi kujisomea, hivyo alisihi waandishi wa habari kujisomea vitabu vilivyozinduliwa ili waweze kutambua mambo yanayokwenda, hivyo kufanya kazi kwa ufanisi.

Mchambuzi wa Kitabu cha State of the Media in Tanzania (Hali ya Vyombo vya Habari, ambaye pia ni mwandishi wa habari mkongwe, Pili Mtambalike, alisema kimeelezea kuhusu sheria, sera na mamlaka zilizopitishwa zikihusiana na fani ya habari.

"Imeelezewa hali ya kutishwa hivyo waandishi kutokuwa na uhakikia wa kuandika habari, pia hali ya ufungiaji wa vyombo vya habari hali imesababisha kuanza kuogopwa," alisema Mtambalike.

Alisema upande wa mafunzo baadhi ya vyuo vya uandishi wa habari vinapokea idadi ndogo ya wananfunzi tofauti na awali, hali ambayo inatokana na utaratibu uliowekwa na serikali wa masharti ya kujiunga na vyuo.

Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, pamoja na kuzunguzia umuhimu wa vitabu vilivyozinduliwa alisema pia kuna mambo mawili yanayomsisimua mojawapo ni ripoti ya 2019 Kimataifa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari iliyoandaliwa na waandishi wasiokuwa na mipaka.

Alisema ripoti hiyo inaonesha kuwa Tanzania imeshuka kwenye viwango vya uhuru wa habari kwa nafasi 25 mwaka jana, ambapo imetoka nafasi ya 93 hadi nafasi ya 118 kati ya nchi zote duniani.

Kajubi alisema hali hiyo ya kuporomoka imejitokeza mfululizo ndani ya mwaka wa tatu mfululizo ambapo Tanzania imekuwa ikishuka kwenye viwango hivyo ambapo mwaka 2016 ilishuka kwa nafasi 12 ilikuwa nafasi ya 83, kabla ya kuwa ya 93 mwaka 2017 ikiwa imeshuka kwa nafasi 10.

Absalom Kibanda alizungumzia kuhusu kitabu cha ubora wa taaluma na maadili ya vyombo vya habari alisema kuwa pamoja na changamoto zinazo wakabili waandishi kuna udhaifu wa kitaaluma.

Alisema miongoni mwa udhaifu huo ni kubainika kuwapo kwa vyombo kadhaa vya habari visivyotumia vyanzo vingi ,kutawaliwa na mfumo dume, visivyojali ulinganifu wa habari za jinsi au vyanzo.

## Shahidi: Zitto alitoa taarifa ya uchochezi

**Na Elizabeth Zaya**

SHAHIDI wa kwanza ambaye ni Mkuu wa Upelelezi mkoa wa Kipolisi Kinondoni (RCO), John Makungu, katika kesi ya uchochezi inayomkabili Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, jana alianza kutoa ushahidi wake na kusema alijiridhisha mshtakiwa huyo kutoa taarifa ya uchochezi.

Shahidi huyo aliielezea Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu namna alivyopata taarifa za uchochezi kutoka kwa Kiongozi huyo ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini.

Akiongozwa na Wakili wa serikali Nassoro Katuga, shahidi huyo alidai Oktoba 28, mwaka jana Zitto alifanya mkutano na vyombo vya habari ofisini kwake na kutoa taarifa za uchochezi dhidi ya Jeshi la Polisi na wananchi.

Makungu alidai tarehe hiyo majira ya jioni akiwa anaperuzi kupitia mtandao wa Youtube aliona taarifa hizo ambazo zilikuwa zikizungumzwa na Zitto kwa vyombo vya habari na hivyo kuwashirikisha watu wake wa uhalifu wa kupitia mitandao (Cyberclime) na wakajiridhisha kuwa alichokuwa akikizungumza ni uchochezi kati ya Polisi na wananchi.

Makungu alisema siku iliyofuata akiwa katika majukumu yake katika Barabara ya Morogoro eneo la Manzese Tiptop, alikuta mkusanyiko wa watu usiokuwa wa kawaida na kwamba aliposhuka alikuta kundi la wananchi wakibishana kwamba Jeshi la Polisi limekuwa la kihuni na kinyama na alipofuatilia aligundua walikuwa wakifuatilia matamko ya taarifa kwa vyombo vya

INAENDELEA UK. 8

SHIRIKA LA UMEME TANZANIA

TANESCO

TAARI FA KWA UMMA
MSAMAHA WA RIBA

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linawataarifu Wateja wake wote kuwa:
Kuanzia Tarehe 1 hadi 31 MEI, 2019 TANESCO itaendesha zoezi la Msamaha wa RIBA kwa wateja wake wote ambao wana madeni ya muda mrefu.

Ili kupata Msamaha wa Riba Mteja mwenye deni la Umeme la muda Mrefu atapaswa kufika katika Ofisi za TANESCO Mkoa au Ofisi za Wilaya, ili kuhakiki deni kamili, na kulipa kiasi chote cha deni lake ndani ya Mwezi mmoja.

Wateja wote wenye Madeni ya umeme mnakumbushwa kutumia fursa hii ili kuweza kulipa madeni yenu kwa wakati na kuondokana na usumbufu wa kusitishiwa huduma ya Umeme.

KUMBUKA: FURSA HII INATOLEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MMOJA TU, (YAANI MWEZI WA TANO TU.)

Imetolewa na: OFISI YA UHUSIANO
TANESCO MAKAO MAKUU

215193202

# TANGAZO

# Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFAZA FEDHA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 Machi 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | | Robo Mwaka ya sasa 31-Mar-19 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 1,512 | 849 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 17,032 | 11,586 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 44,928 | 49,500 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,299 | 9,883 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 8,795 | 4,737 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 70,518 | 69,901 |
| | 12 | Mali Nyingine | 2,938 | 8,593 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 837 | 855 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **149,858** | **155,904** |
| B. | | **B. DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 44,386 | 45,050 |
| | 18 | Amana za Wateja | 68,619 | 68,764 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 | Amana Maalumu | 94 | 5,040 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 43 | 44 |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,876 | 2,197 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| | 27 | Dhima Nyingine | 685 | 360 |
| | 28 | Madeni | - | - |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **115,703** | **121,455** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **34,155** | **34,449** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 2,647 | 1,630 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 8,745 | 7,606 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 591 | 2,346 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 672 | 1,367 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **34,155** | **34,449** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 6,681 | 5,906 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 4,205 | 4,967 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,315 | 1,332 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22.79% | 22.10% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.85% | 6.97% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 63.51% | 59.93% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 47.06% | 44.84% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83.78% | 80.48% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | -4.84% | -11.01% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | -3.88% | -9.89% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 Machi 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka wa sasa 31 Machi 2019 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 Machi 2018 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31 Machi 2019 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 Machi 2018 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,922 | 3,676 | 2,922 | 3,676 |
| 2 Gharama za Riba | 1,246 | 1,439 | 1,246 | 1,439 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,676** | **2,237** | **1,676** | **2,237** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 77 | 261 | 77 | 261 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **221** | **300** | **221** | **300** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 72 | 64 | 72 | 64 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 150 | 236 | 150 | 236 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **989** | **967** | **989** | **967** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 458 | 394 | 458 | 394 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 531 | 573 | 531 | 573 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **831** | **1,309** | **831** | **1,309** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 240 | 300 | 240 | 300 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **591** | **1,009** | **591** | **1,009** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **591** | **1,009** | **591** | **1,009** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 28 | 30 | 28 | 30 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 110 | 188 | 110 | 188 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.21% | 2.92% | 2.21% | 2.92% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 6.85% | 11.66% | 6.85% | 11.66% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 31.46% | 24.33% | 31.46% | 24.33% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.51% | 5.52% | 5.51% | 5.52% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 Machi 2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.01.2019** | 21,500 | - | 9,952 | 1,630 | 1,367 | - | **34,449** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 591 | - | - | - | **591** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (430) | - | - | - | **(430)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,655) | 1,655 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 695 | - | (695) | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | (638) | - | - | **(638)** |
| Mengineyo | | | 184 | | | | **184** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.03.2019** | **21,500** | **-** | **9,336** | **2,647** | **672** | **-** | **34,155** |
| **Mwaka uliopita 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.10.2018** | **21,500** | - | **9,983** | **3,584** | **1,496** | - | **36,563** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | **37** | - | - | - | **37** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | **(202)** | **202** | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | **134** | **(5)** | **(129)** | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | **(2,151)** | - | - | **(2,151)** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.12.2018** | **21,500** | **-** | **9,952** | **1,630** | **1,367** | **-** | **34,449** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 Machi 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2019 | Robo Mwaka iliyopita 31 Desemba 2018 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31 Machi 2019 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31 Machi 2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 831 | 547 | 831 | 1,309 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 139 | (644) | 139 | 278 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,623) | (164) | (1,623) | (3,809) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | (3) | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (5,755) | (14,698) | (5,755) | 4,518 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (1,070) | 6,414 | (1,070) | 2,648 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 48 | (350) | 48 | (86) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 5,655 | 1,228 | 5,655 | (754) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (240) | (510) | (240) | (478) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(2,016)*** | ***(8,180)*** | ***(2,016)*** | ***3,625*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (44) | (529) | (44) | (18) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | 5 | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(44)*** | ***(525)*** | ***(44)*** | ***(18)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | (645) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | - | - | - | ***(645)*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(2,059)** | **(8,705)** | **(2,059)** | **2,962** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 34,685 | 43,391 | 34,685 | 58,311 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **32,626** | **34,685** | **32,626** | **61,273** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2019**

**Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Ashwani Kumar Negi<br>Mkurugenzi Mkuu | Imesainiwa | 04.04.2019 |
| Mr. Poncian Katesigwa<br>Mkuu wa Fedha | Imesainiwa | 04.04.2019 |
| Mr. Allen Richard<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Imesainiwa | 04.04.2019 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Mr. Fredrick Mbala- Mkurugenzi | Imesainiwa | 04.04.2019 |
| 2. Mr. S.K. Mukherjee - Mkurugenzi | Imesainiwa | 04.04.2019 |

## DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| NO. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE USD | CHARGE/FEE TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Current Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 500 | 500,000 |
| b) | **Monthly service fee (breakdown per customer)** | | |
| | Folio Charge | 4 | 6,000 |
| c) | Cheque withdrawal over the counter | | |
| | Up to Tshs 25,000,000 a day | - | free |
| | Over 25,000,000 a day | - | 0.15% of withdrawn amount |
| | Up to 5000 USD a day | free | - |
| | Over 5000 USD withdrawal | 0.6% of withdrawn amount | - |
| d) | Fees per ATM withdrawal | - | - |
| e) | ATM mini statement | - | - |
| f) | Interim/additional statement per page | 1.50 | 1500 |
| g) | Periodic scheduled statement | free | free |
| h) | Cheque book **(50 leaves)** | 27 | 42,000 |
| i) | Dishonoured Cheque | 55 | 70,000 |
| j) | Special clearance | | |
| | Within walking distance 1km | 45 | 70,000 |
| | More than 1km | 65 | 95,000 |
| k) | Counter cheque | - | - |
| l) | Inward/Outward cheque collection-USD | 0.60% Min comm. 18 postages USD 90 | - |
| m) | Cancelation of bankers cheque/DD | 15 | 20,000 |
| n) | | | |
| o) | Stop payment | 28 | 35,000 |
| p) | Standing order | - | - |
| q) | Balance enquiry | free | Free |
| r) | Issue of Balance certificate | 7 | 9,000 |
| s) | New ATM card issuance | - | - |
| t) | ATM card renewal or replacement | - | - |
| u) | Overdrawn account interest charge | - | - |
| | Overdrawn in current account | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| | Overdrawn in loan account | 2% over regular rate | 2% over regular rate |
| | Unarranged overdraft | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| v) | Interbank transfer | - | - |
| w) | Bill payments through ATM | - | - |
| x) | Deposit fee | - | - |
| | **Savings Accounts** | | - |
| | (Up to USD 5000) | Free | - |
| | (Over USD 5000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| | **Current account.** | | |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | | |

**DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014**
**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

| No | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE USD | CHARGE/FEE TSHS |
|---|---|---|---|
| **2.0** | **Savings Accounts** | | |
| a) | Saving bank customer ID Card-one time | 7 | 10,000 |
| b) | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 2,000 | 25,000,000 |
| c) | Cash withdrawal charges over USD 2,000 to 5,000 per day | 0.25% of withdrawal amount | |
| d) | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.60% of withdrawal amount | |
| e) | Cash withdrawal charges over TZS 25,000,000 per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| f) | Required minimum opening balance | | |
| | Without Cheque book | 50 | 50,000 |
| | With Cheque book | 200 | 200,000 |
| g) | Monthly service fee | - | - |
| h) | Interim statement | 1.5 per page | 1500per page |
| i) | Cheque book charges 25 leaves | 15 | 20,000 |
| j) | Account closure | 25 | 35,000 |
| k) | **Maintenance of minimum account balance** | | |
| | Without cheque book | 50 | 50,000 |
| | With cheque book | 200 | 200,000 |
| l) | **Minimum balance charges (in case of non maintenance of minimum balance )** | | |
| | Without cheque book | 4 p.m | 900 p.m |
| | With cheque book | 15 p.m | 3,600 p.m |
| **3.0** | **Current Accounts** | | |
| | Ledger folio charges per folio (40lines per folio) | 4 per folio | 6,000 per folio |
| | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 5,000 | 25,000,000 |
| | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.6% of withdrawal amount | - |
| | Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| | Cheque book charges 50 leaves | 27 | 42000 |
| | Account closure charges | 70 | 85,000 |
| | **Maintenance of minimum account balance** | 500 | 500,000 |
| | **Minimum balance charges** | 15 p.m | 20,000 p.m |
| **4.0** | **Electronic Banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | - | - |
| b) | Internet transfers | - | - |
| c) | SMS banking | - | - |

| | | Minimum SMS Alert Charge ( to be recovered quarterly upfront) | Number of Free SMS on paying SMS Alert charge | SMS Alert charge per SMS beyond the free SMS (To be recovered in monthly basis) |
|---|---|---|---|---|
| d) | SMS Alert facility - | | | |
| | -Individual | USD 3.00 (USD a/c)<br>TZS 5,000 (TZS a/c) | 1st 50 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS<br>TZS 100 per SMS |
| | -Corporate | USD 10.00 (USD a/c)<br>TZS 15,000 (TZS a/c) | 1st 150 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS<br>TZS 100 per SMS |

| No | ITEM/TRANSACTION | USD | | TSHS |
|---|---|---|---|---|
| e) | Others | - | | - |
| **5.0** | **Foreign Exchange Transaction.** | - | | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | | |
| | | A/C holder | Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 | 40 | -- |
| | USD 6001-10,000 | 30 | | -- |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | | -- |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | | - |
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | | |
| **6.0** | **Other Charges** | | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per Activation | | | |
| | -Individuals | 3 | | 5,000 |
| | -Corporate | 6 | | 12,000 |
| **7.0** | **Personal Loans. Charges** | | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | | |
| e) | **Others** | | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | | |
| **8.0** | **Guarantee (Performance/Financial)** | | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | | |
| **9.0** | **Imports** | | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | | |
| **10.0** | **Exports** | | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | | |
| | LC advising charges | USD 150 | | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | | |

No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the period covered by the disclosure

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 04.04.2019 |
| 2. | Poncian Katesigwa | Head of Finance | Signed | 04.04.2019 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 04.04.2019 |

### OTHER DISCLOSURES (VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Base or Prime Lending rate** | 7.00% p.a. | 16.00% p.a. |
| **2.0** | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 4.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| **5.0** | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 6.50% |
| | Over 6 months | 2.50% | 7.50% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 7.00% |
| | Over 6 months | 3.00% | 8.00% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| No. | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 04.04.2019 |
| 2. | Poncian Katesigwa | Head of Finance | Signed | 04.04.2019 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 04.04.2019 |

215193602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mahakama ijitathmini kila wakati kuboresha utendaji

**MAHAKAMA** ni mhimili ambao umekuwa ukielekezewa lawama na raia wengi wa nchi yetu, kikubwa zaidi ni kuchelewesheswa haki.

Haki tunayoizungumzia ni kuhusiana na mashauri mbalimbali ambayo mhimili huo umekuwa ukiyashughulikia, yakigusa pande mbili ambazo ni walalamikaji na walalamikiwa katika kesi zote za aina mbili, yaani za madai na za jinai.

Kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikiikabili mahakama, ndio maana mashauri hayo yamekuwa yakichelewa kumalizwa, hivyo kuwafanya wahusika waathirike kwa namna mbalimbali.

Kimsingi, Mahakama ya Tanzania imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi na kwa muda mrefu. Kubwa ni uhaba wa mahakimu na majaji pamoja na vifaa, ingawa kwa miaka michache iliyopita kuna jitihada zimefanyika na kukabiliana na hali hiyo. Tumekuwa tukishuhudia idadi ya majaji na mahakimu ikiongezwa pamoja na uboreshaji wa miundombinu sambamba na vifaa. Timeshuhudia pia jinsi ulivyoanzishwa mfumo wa matumizi ya Tehama na matumizi yake kusisitizwa kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma.

Hata hivyo, kwa kuwa Mahakama ina wadau wengi, si rahisi kumaliza changamoto zote hususan malalamiko, kwa sababu kila mwenye shauri angependa limalizwe ndani ya siku moja.

Juzi Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alitaja baadhi ya sababu zinazochangia kutotolewa haki kwa wakati mahakamani kuwa ni tabia za uvivu, uchonganishi, ulalamishi, kuchelewa na ubishi usioeleweka.

Alisema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa mwaka wa kutathmini utendaji wa Mahakama ya Rufani.

Prof. Juma alisema majaji wana wajibu mkubwa wa kutoa haki kwa mujibu wa sheria na kutoa uamuzi hata katika mambo yasiyo na sheria. Aliwataka majaji pamoja na kuzingatia sheria na katiba katika kutoa haki, kutosahau masuala ya kiutamaduni ya mahakama na tabia ambazo hazijaandikwa ili kusaidia utoaji wa haki.

Alisema pamoja na kutakiwa kutegemea sheria na katiba, pia yapo mambo ya kiutamaduni na tabia ambazo hazijaandikwa sehemu yoyote, hivyo wanapaswa kuyazingatia katika kutoa haki. Alisema wanatakiwa kuwa na uelewa wa sheria kwa sababu wananchi wanategemea watapata haki kutoka kwao, tena kwa wakati.

Aliongeza kuwa upo mkakati wa miaka mitano wa mahakama unaojenga tabia ya kutoa haki kwa kutumia utamaduni.

Tunaishauri Mahakama ya Tanzania kujenga utamaduni wa kujitathmini kila wakati kuhusiana na malalamiko yanayotolewa na raia dhidi yake na kufanya marekebisho yakiwamo maboresho ili kukidhi mahitaji ya wananchi.

Jambo la kupongeza ni utamaduni ambao umejengeka miongoni mwa viongozi wakuu wa mahakama hiyo, akiwamo Jaji Mkuu kila wakati kuhimiza utendaji bora miongoni mwa watendaji na watumishi.

Mara nyingi tunawasikia au kuwaona majaji wakihimiza usikilizaji kesi kwa wakati na kutenda haki. Hatua ya kukumbuka ni kuwa mwaka juzi Jaji Mkuu aliwataka majaji kutokwenda likizo kwa ajili ya kukamilisha mashauri yaliyokuwa mbele yao.

Kadhalika, tunaona kwamba ni vizuri kwa viongozi wakuu wa Mahakama ya Tanzania kujikita zaidi katika kuhimiza majaji na mahakimu kutenda haki bila upendeleo wa aina yoyote.

Hilo nalo ni miongoni mwa mambo ambayo Jaji Mkuu aliyagusia juzi, kwa kusema kuwa watoa haki wasikubali kuingiliwa na mtu yeyote katika majukumu yao ya kutoa haki.


Mahakama itabaki na heshima yake pamoja na kuaminiwa na raia wote, ikiwa watumishi na watendaji wake watakuwa huru na vile vile kutojiingiza katika itikadi za kisiasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

Na Yasmine Protace

# Si wakati wa kuchekea uchafuzi wa mazingira

**UTUNZAJI** mazingira unatakiwa kuangaliwa na kila Jamii, katika kila mahali. Hapo lengo ni kuepuka matatizo ya kiafya inayoweza kuikabili sehemu husika .

Kuna baadhi ya maeneo ambayo kwa kawaida, kila ukipita, unakuta taka zimetupwa ovyo, pembezoni mwa barabara huku mama lishe wakiendelea na biashara zao za vyakula.

Kitendo cha kutupwa taka ovyo barabarani na biashara za vyakula zinapoendelea kutolewa katika maeneo hayo, kunachangia magonjwa ya milipuko kwa walaji na wasio walaji, lakini wanakuwa wanahusika kwa namna moja au nyingine.

Hivi karibuni, Hilda Kirasisa, ambaye ni Mwenyekiti wa Asasi Isiyo ya Kiserikali ya Utafiti wa Masuala ya Kinsia, kwa Ajili ya Kumbukumbu na Masuala ya Kimaendeleo ((WRDP), alianza kutafsiri mazingira kuwa ni vitu vinavyozunguka mandhari ya uhai, zikiwamo hewa, ardhi na maji.

Hilda aliyekuwa akitoa mada katika Semina ya Maendeleo ya Kijinsia (GDSS), anaeleza historia yake kwamba alishatumikia Wizara ya Maji na Umwagiliaji na waligundua ukosefu wa elimu kwa baadhi ya jamii kuhusiana na masuala ya mazingira imechangia kwa kiasi kikubwa vyanzo vya maji, ikiwamo uchafu mitaani na barabarani.

Anasema watu wanadhani uharibifu wa mazingira pekee unaathiri afya za walaji, lakini wamesahau uharibifu huo wa mazingira unaenda mbali kusababisha ulemavu.

Hilda anasema, suala la mazingira linatakiwa kuangaliwa kwa upana hata katika vyoo shuleni, kama miundombinu yake ipo rafiki au la, kwani inachangia kuwakwaza walemavu wasihudhurie masomo..

Anatoa mfano, alipokuwa mtumishi katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji, alitembelea maeneo mbalimbali ya nchi na akabaini changamoto katika masula ya maji na miundombinu.

Anasema kipindi ambacho mvua inanyesha, baadhi ya watu hukosa ustaarabu kwa 'kutapisha' maji machafu, wanakoosha magari katika vyanzo vya maji.

" Watu wanaosha magari katika mito ambayo kuna wakulima, wamelima mboga, pia jamii ikazitumia mboga hizo kunauwezekana mkubwa mtu kupata kansa," anasema mama huyo.

Anaongeza kwamba vyanzo vingi vya maji vinaingia mtoni, ambako mifugo inakunywa, Hali hiyo inasababisha watu kuugua maradhi ya tumbo.

Hilda anatoa mfano wa soko mojawapo katika Manispaa ya Ubungo, kwamba linachanganya wafanyabiashara wa mkaa, mama lishe, vyakula na matunda, hali ambayo ni hatari.

Anasema, kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaohifadhi ndizi katika matope katika kipindi cha mvua katika soko hilo, ambako pia watu wanaosha miguu yao.

Mtaalamu huyo wa mazingira, anakumbusha kuwa ni makosa makubwa kisheria, ambayo hatua zinapaswa kuchukuliwa, vinginevyo magonjwa ya milipuko yatachukua nafasi yake.

Nini kifanyike? Hata Hilda anasema viongozi wa mitaa wanawajibika kuwachukulia hatua waosha magari katika vyanzo vya maji.

Ofisa Afya wa Soko la Mabibo, Jacobo Mwakalonga, anakana malalamiko hayo, akisema suala la afya sokoni wanalizingatia.

Pia, kuhusu mamalishe wanaofanya biashara jirani na wauza mkaa, anaeleza uongozi wa soko ulishawaandikia barua za kuondoka katika maeneo na waingie ndani ya soko kufanya biashara zao.

Anasema, mikakati ya kuwahamisha inaendelea na uongozi wa soko umeshaandaa mabanda ya kuwawezesha kupika mahali salama.

Mwakalonga, pia anawazungumzia waosha miguu, kwamba anafuatilia ukweli wake, kwani alifahamu kwamba maji wanayotumia ni kutoka mabomba ya sokoni.

Wadau wa GDSS, nao wanadai kuwapo kila haja ya viongozi wa serikali za mitaa kusimamia sheria za umwagaji maji machafu katika makazi ya watu.

Amina Juma, ni mdau wa GDSS anayesema katika kipindi cha mvua, baadhi ya watu wanatumia mwanya kumwaga maji machafu.

Ushauri wake, ni viongozi wasiwaonee aibu wachafuzi wa mazingira, bali wawachukulie hatua za kisheria, ili kukomesha nyendo hizo.

# Raia Nigeria, Lativia kesi ya ' unga'

**Na Elizabeth Zaya**

RAIA watatu wa kigeni akiwamo anayedaiwa kuwa mchungaji, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi kwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin, kilogram 4.87.

Washtakiwa hao ni Linda Mazure( 21) mwanafunzi na raia wa Lativia, Henry Ogwuanyi (44) mfanyabiashara na raia wa Nigeria na anayedaiwa kuwa ni mchungaji, pamoja na Martins Plavins (20) mkandarasi na raia wa Lativia.

Wakili wa Serikali, Batilda Mushi, alidai Aprili 24, mwaka huu washtakiwa hao wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 33/ 2019.

Akiwasomea hati ya mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi, Augustine Rwizile, Mushi alidai washtakiwa kwa pamoja wanakabiliwa na shtaka moja la kusafirisha dawa hizo.

Mushi alidai kuwa washtakiwa hao wanadaiwa kutenda kosa hilo, April 17, 2019 katika uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere ( JNIA). Alidai siku hiyo walikutwa wakisafirisha kilogramu 4.87 za dawa za kulevya aina ya Heroin kinyume cha sheria ya kuzuia na kupambana na dawa za kulevya.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kutokana na Mahakama ya Kisutu kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi isipokuwa kwa kibali maalumu.

"Washtakiwa hamtakiwi kujibu chochote mahakamani hapa kwa sababu mahakama hii haina uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi isipokuwa kwa kibali maalumu," alisema Hakimu Rwizile.

Mushi alidai upelelezi wa shauri hilo haujakamilika, hivyo wanaomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Rwizile aliahirisha kesi hiyo hadi Mei 7, mwaka huu kesi hiyo itakapotajwa na washtakiwa wamerudishwa rumande kutokana na kesi inayowakabili kutokuwa na dhamana kwa kujibu wa sheria.

Katika tukio jingine, Raia wawili wa Nigeria, Henry Ogwuanyi (44) na Onyebuchi Ogbu (34), walifikishwa katika Mahakama hiyo wakikabiliwa na shtaka la kukutwa na dawa za kulevya.

Wakili wa Serikali, Constantine Kakula, alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi kuwa washtakiwa hao wanadaiwa kutenda kosa hilo April 21, mwaka huu, katika mtaa wa Msimbazi, Kariakoo Dar es Salaam.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa siku hiyo, katika eneo hilo walikutwa na dawa za kulevya aina ya heroini kilogramu 15.8, kinyume cha sheria.

Washtakiwa hawakutakiwa kusema chochote kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi hiyo. Hakimu Shaidi aliahirisha kesi hiyo hadi Mei 8, mwaka huu itakapotajwa na washtakiwa walirudishwa rumande.

# Ushahidi zaidi Jamhuri dhidi ya kina Malinzi leo

**Na Elizabeth Zaya**

KESI ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji fedha, inayomkabili aliyekuwa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi na wenzake wanne, imepangwa kuendelea na usikilizwaji leo upande wa Jamhuri.

Washitakiwa hao walipanda kizimbani jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mbele ya Hakimu Mkazi Augustina Mmbando, wakati shauri hilo lilipopelekwa kwa ajili ya kuendelea na usikilizwaji ushahidi upande wa Jamhuri.

Hata hiyo, kesi hiyo ilishindwa kuendelea na usikilizwaji jana kutokana na Hakimu anayeendesha kesi hiyo kuwa na udhuru.

Wakili kutoka Taasisi ya Kuzua na Kupambana na Rushwa( TAKUKURU), Leonard Swai, alidai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Augustina, wakati shauri hilo lilipopelekwa kwa ajili ya kuendelea na usikilizwaji.

Awali, Swai alidai shauri lilipelekwa kwa ajili ya kuendelea na usikilizwaji lakini alipata taarifa kwamba Hakimu Mkazi Mwandamizi Maira Kasonde anayeendesha kesi hiyo kuwa na udhuru, hivyo anaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Baada ya kudai hayo, Wakili wa utetezi Richard Rweyongeza, alidai hana pingamizi na hilo.

Hakimu Augustina, baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili, alisema kesi hiyo itaendelea na usikilizwaji upande wa Jamhuri leo.

Tayari mashahidi 13 wa upande wa Jamhuri wameshatoa ushahidi dhidi ya Malinzi akiwamo aliyekuwa dereva wake.

Mbali na Malinzi aliyekuwa ni Rais wa (TFF), washitakiwa wengine ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa TFF, Selestine, Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga, Meneja wa TFF Miriam Zayumba na Karani Flora Rauya.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka 30 katika kesi ya jinai namba 213 ya mwaka 2017 yakiwemo kughushi, kula njama, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji fedha za Marekani 173, 334.

Kabla ya Hakimu Kasonde shauri hilo lilikuwa mbele ya Hakimu Wilbard Mashauri ambaye aliteuliwa na Rais John Magufuli kuwa Jaji wa Mahakama Kuu, hivyo kesi hiyo imepangwa kwa Hakimu Mkazi Maira Kasonde.

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wako rumande kwa kukabiliwa na mashitaka ya utakatishaji wa fedha kuwa miongoni mwa mashtaka ambayo kwa mujibu wa sheria hayana dhamana huku wenzao Miriam na Flora wapo nje kwa dhamana.



Mamalishe akiandaa ugali kwa ajili ya mlo wa mchana kwa wateja wake, katika Mtaa wa Tandamti, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# CAG abaini uhaba wa zahanati, vituo vya afya

**Na Enock Charles**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini kuwapo kwa changamoto ya uhaba wa zahanati na vituo vya afya nchini.

Vilevile, mtaalamu huyo wa ukaguzi wa hesabu amesema amebaini kuwapo kwa changamoto ya uhaba wa watumishi 48,710 kwenye halmashauri 314 katika miradi ya sekta za kilimo, afya na maji, alieleza kuwa upungufu huo unaathiri utekelezaji wa ufanisi wa miradi. Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18, Prof. Assad anabainisha kuwa tathmini yake ya Mpango Kabambe wa Afya kwa mwaka wa fedha 2017/18 pamoja na taarifa za kila robo mwaka za utendaji (za kifedha na kitaalamu), imebaini upungufu wa miundombinu ya vituo vya afya nchini. Katika ripoti yake hiyo, CAG Assad anasema amebaini halmashauri zina upungufu wa zahanati 109, vituo vya afya 32, nyumba za watumishi 63 na wodi 45.

Prof. Assad pia anabainisha kuwa magari 31 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania katika halmashauri 31 yamechakaa na kukaa kwa muda mrefu kwenye karakana bila kufanyiwa matengenezo au kuuzwa kama inavyotakiwa kisheria.

"Kwa mujibu wa ripoti hiyo agizo 45(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Aya ya 26 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma, magari hayo hutakiwa kufanyiwa matengenezo au kuuzwa ili yasiendelee kuchakaa zaidi, kwa kuwa magari yaliyochakaa huathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania," anabainisha.

# Waziri asaidia vifaranga 23,000 jimboni

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amekabidhi vifaranga vya kuku 23,000 vya nyama na mayai wenye thamani ya Sh. milioni 68 kwa ajili ya vikundi vya wafugaji kuku jimboni kwake.

Makabidhiano hayo yalifanyika jana katika ofisi za Jiji la Dodoma ambapo Mbunge huyo alimkabidhi mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma Prof, Davids Mwamfupe, vifaranga hivyo pamoja na vifaa vingine kwa niaba ya vikundi hivyo na kuhudhuriwa na madiwani wa jimbo hilo.

Mavunde alikabidhi vifaranga 23,000 pamoja na vifaa vingine kwa ajili ya vikundi 37 vya uzalishaji mali kwenye jimbo lake kupitia mfuko wa jimbo.

Alisema mradi huo unalengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi hasa akinamama na vijana kupitia vikundi vyao vya uzalishaji mali vya jimboni.

Mavunde alisema mradi huo utawawezesha wananchi wa jimbo lake kuitumia fursa ya Serikali kuhamia Dodoma kujiongezea kipato.

Alibainisha kuwa kwa kupitia mfuko huo wa jimbo vikundi 37 kwenye kata 36 za jimbo hilo vitapata msaada huo wa vifaranga vya kuku aina ya kroiler.

Alivitaja vifaa vingine alivyokabidhi kwenye vikundi hivyo kuwa ni vyombo vya kuweka maji na chakula cha kuku , chanjo pamoja na mifuko ya chakula cha kuku kwa muda wa mwezi mmoja kwa kila kikundi.

Hata hivyo, alisema hivi karibuni atakabidhi mabwawa ya samaki kwa baadhi ya vikundi vya jimbo hilo vilivyoomba kupitia mfuko wa jimbo.

Afisa Takwimu wa Jiji la Dodoma, Debora Mwinje, alisema halmshauri hiyo ilipokea fedha kiasi cha Sh. 68.5 kutoka mfuko wa kuchochea maendeleo ya jimbo la Dodoma mjini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo

Hata hivyo, alisema Halmashauri ya Jiji ilitoa tangazo lililowataka kila kata ilete mradi utakaotekelezwa na mfuko wa jimbo na kata 37 zilileta maombi kati ya 41 za Jimbo hilo,miradi iliyopendekezwa ni ufugaji kuku na samaki kwa vikundi.

Alisema baada ya kupitia maandiko yao vikundi 37 vilikidhi vigezo vya kupewa msaada huo ambao jana Mbunge alikabidhi rasmi.

Kwa upande wake, Meya Prof. Mwamfupe alimshukuru Mbunge huyo kwa kutoa msaada huo ambao utawakwamua wananchi kiuchumi.

"Msaada huu ni chachu, tunaomba madiwani wenzangu mkawahamasishe wananchi kusimamia vizuri mradi huu ili kuepuka kurudi nyuma," alisema.

# Kesi ya Mdee yapigwa kalenda

**Na Elizabeth Zaya**

KESI ya kutoa lugha chafu dhidi ya Rais John Magufuli inayomkabili Mbunge wa Kawe, Halima Mdee (Chadema), imeshindwa kuendelea na ushahidi kutokana na Hakimu anayeendesha shauri hilo kupata udhuru.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Patric Mwita, aliieleza mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa shauri hilo lilikuja kwa ajili ya kusikilizwa hivyo aliiomba mahakama hiyo iahirishe shauri hilo kwa kuwa hakimu anayeendesha shauri hilo amepata udhuru

"Upande wa mashtaka tulikuwa na shahidi, tunae shahidi Abdi Chembeya kutokana na hakimu anayeendesha shauri hilo kupata udhuru, hivyo tunaiomba mahakama hiyo ipange tarehe nyingine" alisema Patric

Baada ya maelezo hayo Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, aliahirisha shauri hilo hadi Mei 15, mwaka huu na mshtakiwa yupo nje kwa dhamana.

Mpaka sasa mashahidi watatu wa upande wa mashitaka wameshatoa ushahidi katika kesi hiyo akiwamo Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Urafiki, Mrakibu wa Polisi (SP) Batseba Kasanga.

Katika kesi ya msingi inadaiwa kuwa Julai 3, 2017 katika ofisi za makao makuu ya Chadema zilizopo Mtaa wa Ufipa wilayani Kinondoni, Mdee alitamka maneno dhidi ya Rais John Magufuli kuwa, 'anaongea ovyo, anatakiwa afungwe breki,' kitendo kinachodaiwa kuwa ni kumdhalilisha Rais na kusababisha uvunjifu wa amani.



Wachuuzi wa machungwa wakiwa wamejipumzisha wakati wakisubiri wateja katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shahidi: Zitto alitoa taarifa ya uchochezi

**INATOKA UK. 4**

habari iliyotolewa na Zitto.

"Ilibidi nimuite mtu mmoja aliyejitambulisha kwa jina la Shabani Hamisi aliyekuwa katika kundi lile na nilipomuuliza walichokuwa wakibishania, aliniambia kwamba walikuwa wanajadili hotuba ya Zitto," alidai Makungu na kuongeza:

"Baada ya hapo niliondoka hadi Kimara Korogwe kituo cha mabasi nako nilikutana na kundi lingine lenye watu wengi walioonekana kuwa na ghadhabu wakilijadili Jeshi la Polisi ni la kinyama na pia nilizungumza na kijana Mashaka Juma na kuchukua namba yake ya simu."

Alidai baada ya kupata taarifa hizo aliporudi ofisini kwake aliita wataalamu wa makosa ya mtandaoni kujadili suala hilo pamoja na kuwashirikisha makachero kufuatilia taarifa hizo zilizotolewa na Zitto na kuanza upelelezi.

Zitto alifikishwa makahani hapo Novemba 2, mwaka jana akikabiliwa na mashtaka matatu ya uchochezi katika kesi ya jinai namba 28/2018 katika mkutano na waandishi wa habari.

Katika kesi ya msingi, Zitto anadaiwa kutenda makosa hayo Oktoba 28, mwaka jana katika mkutano huo.

Kesi hiyo inatarajia kuendelea kutolewa ushahidi leo katika Mahakama hiyo ya Kisutu.

Aidha, wakati akijieleza Makungu alibanwa maswali kuhusu kiwango chake cha elimu kutoka kwa Wakili wa Utetezi Peter Kibatala.

**Kibatala:** Kabla sijaanza kukuhoji mengine naomba kufahamu elimu yako

**Shahidi:** Darasa la saba

**Kibatala:** Ulimaliza mwaka gani na wapi?

**Shahidi:** Miaka ya tisini

Kibatala: Acha utani, naomba uniambie ulisoma shule gani, wapi na lini ulimaliza.

**Shahidi:** Mwaka 1990.

**Kibatala:** Unajua maana ya press release?

**Shahidi:** Ndio.

**Kibatala:** Ni tukio au nyaraka?

**Shahidi:** Tukio.

**Kibatala:** Na nyaraka inayotolewa kwa waandishi wa habari inaitwaje?

**Shahidi:** Ni nyaraka ya press release.

**Kibatala:** Umesema Zitto Kabwe anajipambanua kama Kiongozi wa ACT unamaanisha nini?

**Shahidi:** Anajitangaza.

# NSSF yafunguka ulipaji wa mafao

**INATOKA UK. 2**

taarifa kutoka kwa wanafamilia kuwa huyu hajafariki au alishafariki dunia, hivyo wanaomba malipo yasitishwe, lakini familia husika haijatoa taarifa na ukifuatilia unakuta ni kweli.

"Unakuta marehemu alikuwa na wake wawili au nyumba ndogo na wote wanataka kulipwa mafao, na wengine hutengeza hadi nyaraka, sasa usipokuwa makini unaweza kulipa fedha kwa wasiostahili," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema hivi karibuni, kitengo cha usalama kilibaini udanganyifu uliofanywa na mwanamke mmoja mkoani Tabora kudai mafao ya mumewe kwa madai kuwa amefariki dunia, na walipofuatilia walibaini hawakuwa wanaishi pamoja na mwanamume hajafariki dunia.

"Yule mama alikuwa na nyaraka zote ambazo ni za kutengeneza, kwa mazingira hayo unaweza kuingia 'mkenge' na kumlipa wakati nyaraka ni feki, tulichokifanya tumewakabidhi polisi washughulike naye," alisema.

Aliongeza kuwa katika kulipa mafao ya warithi, ni lazima kuwe na nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na cheti cha kifo kilichotolewa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita) pamoja na viambatisho vyote.

Erio alisema NSSF inafuatilia kwa karibu kila nyaraka inayowasilishwa kwake na hawapendi kuendelea kuwapo kwa malalamiko ya wanachama, bali kila mmoja kupata huduma kwa mujibu wa sheria.

Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2018 iliboresha mafao ya warithi kwa kuwa na kipengele kinachotamka kuwa mara baada ya mwanachama/mstaafu kufariki dunia na endapo mwanachama atafariki dunia akiwapo kazini na amechangia miezi 180 (miaka 15), wategemezi wake watalipwa mafao ya kifo.

Kanuni za sheria hiyo zimeweka utaratibu wa kulipa mafao hayo kuwa ni mjane au mgane atalipwa asilimia 40 na kama wapo zaidi ya mmoja, yatagawanywa.

Vilevile, watoto watalipwa asilimia 60 iliyobakia na yatagawanywa sawa kwa watoto wote, na kama hakuna watoto, mjane au mgane atalipwa asilimia 100.

Kanuni hizo zimebainisha kuwa kama hakuna mjane au mgane, watoto watalipwa asilimia 100, na kama kuna watoto wapo shuleni, mgawanyo kwa watoto utagawanywa nusu kwa nusu, na nusu moja itatumika kulipia ada na itasimamiwa na mfuko wakati nusu nyingine itagawanywa sawa kwa watoto, huku mahakama ikipewa nafasi ya kubadili utaratibu huo.

Oktoba 20, 2017, serikali ilipitisha uamuzi wa kuunganisha mifuko ya pensheni ya PSPF, LAPF, GEPF na PPF kuunda mfuko wa PSSSF kwa ajili ya watumishi wa umma na kufanya marekebisho kwenye sheria iliyoanzisha Mfuko wa NSSF ili mfuko huo uwe wa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

Sheria ya PSSSF ilipitishwa na Bunge Januari 31, mwaka jana, na kutiwa saini Februari 8, mwaka jana na kutangazwa kwenye gazeti la serikali toleo namba 9 Februari 2018.

Sheria hiyo ilianza kutumika Agosti Mosi, mwaka jana na ndiyo ilikuwa tarehe rasmi ya kuanzishwa kwa Mfuko wa PSSSF.

Hata hivyo, uliibuka mjadala wa kikokotoo lakini Desemba 28, mwaka jana, Rais John Magufuli aliwataka wadau kuendelea na majadiliano hadi mwaka 2023 wakati kikokotoo cha zamani kikitumika.

HABARI KITAIFA

# Iringa yaita w'biashara wake kujerea nyumbani

**Na George Tarimo,** IRINGA

SERIKALI Mkoani Iringa, imewaomba wafanyabiashara wenyeji wa Mkoa wa Iringa kurudi kuwekeza nyumbani kwa kuwa sasa usafiri utakuwa rahisi na wa uhakika. Ombi hilo limetolewa na Mkuu wa mkoa huo, Ally Hapi, baada ya Shirika la Ndege Nchini (ATCL) kutangaza kuanza safari za ndege za shirika hilo katika kiwanja cha ndege cha Iringa kuanzia April 29, mwaka huu.

Mwaka jana serikali ilitangaza kukarabati viwanja vya ndege nchini kikiwamo kiwanja cha ndege cha Iringa ambapo mkuu huyo wa mkoa aliishukuru serikali na wadau walioshirikiana kujenga miundombinu ya kiwanja hicho.

Kiwanja hicho kimekarabatiwa njia ya kuruka na kutua ndege pamoja na kujenga majengo mawili ya abiria wanaoingia na kutoka katika kiwanja hicho, na kuwaomba wawekezaji kutumia fursa hiyo kuwekeza katika sekta mbalimbali mkoani hapo ikiwamo ya utalii.

Hapi alisema kuwa jengo peke yake na kuweka mitambo fedha za wadau umegharimu zaidi ya Sh.milioni 400.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi, alitangaza neema hiyo kwa wasafiri wanaotumia kiwanja cha ndege cha Iringa na kusema kwamba gharama za usafiri wa ndege zitashuka kutoka Sh. 1,000,000 kwa safari ya kwenda na kurudi hadi kufikia Sh. 280,000.

"April 29 mwaka huu ndege ya kwanza ATCL itatuwa Iringa hivyo ukilinganisha na mpango wetu wa biashara Iringa itakuwa imekwenda mbele na miaka miwili kwa maana tulikuwa tunazungumzia mwaka 2022 kwa kuangalia mpango wa ukarabati ulivyokuwa unaendelea, lakini kwa juhudi zake mkuu wa mkoa ameweza kufanya kazi na wadau wake na kutuondoa kwenye mpango wetu wa miaka miwili na hatma kumalizika kwa mwaka huu." alisema Matindi.

Kwa upande wake mwakilishi wa mkurugenzi wa mamlaka ya anga (TAA), Alexander Kalumbete, alisema juhudi za viongozi wa mkoa huo ndizo zimewezesha kuharakisha ukarabati wa kiwanja hicho, na kwamba serikali itaendelea na mipango yake ya kufanya maboresho kwa kadiri bajeti inavyoelekeza.

# Mimba shuleni sasa tishio Kahama

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

JUMLA ya wanafunzi wa kike 26 wamelazimika kukatisha masomo yao kutokana kupata ujauzito katika shule za sekondari za serikali zilizopo katika Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga katika kipindi cha kuanzia Januari 2019 hadi sasa.

Mkuu wa wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliliambia baraza la madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Kahama kuwa tatizo la mimba kwa mwaka huu linaonekana kuwa kubwa zaidi.

Alisema mwaka 2018 wanafunzi wa kike walioripotiwa kupata ujauzito walikuwa ni 21 na kwamba wapo wazazi, viongozi na walimu ambao wamekuwa wakikwamisha watuhumiwa waliosababisha mimba hizo wasikamatwe.

"Bado tatizo la mimba katika shule zetu hasa sekondari lipo kwa wingi, mwaka jana 2018 wanafunzi wa kike waliopata , mimba ni 21, ila mwaka huu 2019, robo ya kwanza tu tayari wanafunzi wa kike 26 wameacha masomo kwa sababu ya mimba na wapo wazazi na walimu wanapoteza ushahidi wa watuhumiwa," alisema DC Macha.

Hata hivyo, Macha aliwataka madiwani na viongozi wengine wa serikali kushirikiana na serikali katika kukabiliana na changamoto hiyo ikiwamo kuwakamata wanaume na wazazi wanaosababisha mwanafunzi wa kike kupata ujauzito.

Macha aliwaonya wazazi na walezi pamoja na wananchi wengine wanaokwepesha ushahidi wa kesi za mimba kwamba serikali itaanza kushughulika nao kwa kuwachukulia hatua kali za kisheria.

# Magufuli aenda ziarani Malawi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli leo ameondoka nchini kwenda Malawi ambako anafanya ziara rasmi ya kiserikali ya siku mbili kwa mwaliko wa Rais wa Malawi, Prof. Arthur Peter Mutharika.

Rais Magufuli akiwa na mkewe, Janeth Magufuli, waliondoka jana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam na walitarajiwa kupokelewa na mwenyeji wao katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kamuzu Mjini Lilongwe.

Akiwa Mjini Lilongwe, Rais Magufuli ataweka shada la maua katika mnara wa kumbukumbu ya aliyekuwa Rais wa Malawi Hayati Bingu Mutharika, kisha atafanya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais Mutharika, na jioni alitarajiwa kuhudhuria dhifa ya kitaifa aliyoandaliwa kwa heshima yake na Rais Mutharika.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Rais Magufuli atamaliza ziara yake kwa kufungua msimu wa Soko la tumbaku na kuzungumza na wadau wa zao hilo na baadaye atarejea nchini, kisha ataanza ziara ya kikazi ya siku nane katika Mkoa wa Mbeya.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kulia), akikabidhi chandarua kwa Peter Shayo, kwa wazazi waliohudhuria kliniki katika kituo cha afya Makole, jijini Dodoma jana, baada ya kuzindua Wiki ya Kupinga Malaria Duniani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mashahidi 6 kujenga kesi ya ubakaji mwanafunzi

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MKAZI wa Kibingo Kata ya Kibirizi Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Yasini Shabani (21), amependishwa kizimbani akikabiliwa na makosa mawili ya kubaka na kumpa ujauzito msichana mwenye umri wa 17 ambae ni mwanafunzi wa darasa la sita.

Mshtakiwa huyo alipandishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma na kusomewa shtaka ambalo anadaiwa kumtendea kitendo hicho mwanafunzi huyo wa Shule ya Msingi Nyatole.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Flora Mtarania, na alikana kuhusika na makosa, na yuko nje kwa dhamana.

Akimsomea maelezo ya awali, Wakili wa serikali, Antia Julius, alidai kuwa mwaka 2018 mwanafunzi huyo alikuwa anasoma darasa la sita katika Shule ya Msingi Nyatole.

Julius aliongeza mwaka 2018 mshtakiwa alianza mahusiano na mwanafunzi huyo, na alifanya nae mapenzi mara kadhaa, hivyo kumpa mimba.

Aliendelea kuieleza mahakama kuwa wazazi baada ya kubaini kuwa mtoto wao ana mimba, walikwenda kutoa taarifa kituo cha polisi na mlalamikaji alipewa PF3 na kwenda hospitalini kwa ajili ya uchunguzi.

Aidha, alidai baada ya upelelezi wa polisi, mshtakiwa alikamatwa na alipohojiwa alikiri kufanya mapenzi na msichana huyo mwaka 2018.

Alidai baada ya upelelezi wa polisi kukamilika, mshtakiwa alifikishwa mahakamani.

Julius aliiambia mahakama kuwa upande wa mashtaka unatarajia kupeleka mashahidi sita na vielelezo viwili, na kuomba mahakama kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu Mtarania aliahirisha kesi hiyo hadi April 30, mwaka huu kwa ajili ya kuanza kusikiliza kesi hiyo.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola akisisitiza kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali kushughulikia makosa ya jinai, ikiwemo kufanya uchunguzi dhidi ya tuhuma husika na kubaini ukweli, katika kikao cha Bunge, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MAELEZO**

# Matumizi ya gesi Dangote kwa siku yawekwa bayana

BUNGE limeelezwa kuwa hadi kufikia Aprili mwaka huu kiwanda cha Saruji cha Dangote kimeanza kutumia gesi wastani wa futi za ujazo milioni tano kwa siku kwa kuzalisha umeme, huku futi za ujazo milioni 15 hadi 20 zikitumika kwa siku kuzalisha saruji.

Aidha, serikali imetenga gesi futi za ujazo Trilioni 8 kwa ajili ya viwanda.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Katika swali lake, alihoji ni lini kiwanda cha Saruji cha Dangote kitapewa gesi asilia na Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC).

Akijibu, Mgalu alisema kuwa Serikali kupitia TPDC imekamilisha kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gesi asilia katika mitambo ya kuzalisha umeme wa muda katika kiwanda cha saruji cha Dangote.

Alieleza kiwanda hicho kimepelekewa gesi hiyo umbali wa mita 100 kutoka katika toleo la kwanza la gesi (Block Valve Station no.1-BVS1).

Alifafanua kuwa, awamu ya kwanza ya mradi wa kuwezesha matumizi ya gesi kuzalisha umeme kwa kiwanda cha Dangote ili kamilika na kuanza kufanya kazi ilifanyika Agosti 2018.

Alibainisha hadi kufikia Aprili 2019 kiwanda hicho kimeanza kutumia wastani wa futi za ujazo milioni tano kwa siku kwa kuzalisha umeme. Aidha, alisema awamu ya pili ya mradi inahusu ujenzi wa miundombinu ya bomba la kusafirishia gesi asilia kutoka BVS 1 kwenda kwenye kiwanda cha Dangote umbali wa kilometa 2.7 kwa ajili ya kuwezesha gesi asilia kutumika kama nishati ya kuchoma malighafi za kuzalisha saruji.

"Jumla ya gharama za mradi ni Sh. bilioni 8.2 na awamu ya pili ya mradi ilikamilika Desemba 2018 na sasa kiwanda cha Dangote kinatumia gesi ya wastani wa futi za ujazo milioni 15 hadi 20 kwa siku kwa ajili ya uzalishaji wa saruji.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema pamoja na kupeleka gesi katika kiwanda hicho lakini kuna viwanda vingine Mtwara ikiwamo vya kubangua korosho na kuhoji serikali ina mkakati gani wa kupeleka gesi kwenye viwanda hivyo.

"Je, usambazaji wa gesi majumbani, serikali ina mkakati gani kwa kuwa matumizi ya gesi ni madogo licha ya kuzalishwa kwa wingi, sasa serikali ina mpango gani wa kuongeza watumiaji kwa Wilaya ya Nanyamba, Masasi na mikoa mingine," alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri huyo alisema serikali inatambua umuhimu wa gesi kwenye viwanda na hadi sasa kuna viwanda 27 vinavyotumia gesi.

Pia, alisema kuna mradi unatekelezwa kwa sasa wa kusambaza gesi viwandani na majumbani hasa maeneo ya Mtwara na Mkuranga na hadi sasa TPDC imekamilisha mazungumzo na mkataba wa mauziano ya gesi ya viwanda viwili vya Mkuranga.

"Kwa upande wa viwanda vya kubangua korosho, naomba niwataarifu wawekezaji wetu wote walio na viwanda kwa ukanda ambao bomba la gesi limepita waje wazungumze na TPDC fursa hiyo ipo," alisema.

Kadhalika, alisema gesi futi za ujazo trilioni 8 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya viwanda tu. "Kwa sasa ununuzi wa vifaa mbalimbali vinanunuliwa kwa ajili ya kusambaza gesi majumbani na ununuzi wa vifaa utakamilika Mei, mwaka huu," alisema.

# NEC kuhakiki majimbo ya uchaguzi

SERIKALI imesema Tume ya Taifa ya uchaguzi(NEC), inatarajia kuhakiki tena majimbo ya uchaguzi wa ubunge Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Zanzibar.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana), Anthony Mavunde, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nungwi(CUF),Yussuf Haji Khamis, aliyetaka kujua ni lini Tume ya Taifa ya Uchaguzi itafanya uhakiki wa majimbo ya ubunge Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema mara ya mwisho NEC ilifanya uhakiki wa majimbo ya uchaguzi wa ubunge mwaka 2015 kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Alibainisha kuwa baada ya uhakiki jumla ya majimbo 26 yalianzishwa kutokana na maombi 77 yaliyowasilishwa Tume kutoka Halmashauri 37 na majimbo ya uchaguzi 46.

"Kwa mujibu wa ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya uchaguzi imepewa jukumu la kuchunguza mipaka ya kiutawala na kuigawa katika majimbo ya uchaguzi wa ubunge," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa kuzingatia ibara hiyo Tume imepewa jukumu la kuchunguza na kugawa majimbo ya uchaguzi ya ubunge mara kwa mara na angalau kila baada ya miaka 10.

"Hivyo, Tume ya Uchaguzi inatarajia kuhakiki tena majimbo ya uchaguzi wa ubunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Zanzibar baada ya kutangaza kufanya hivyo kwa mujibu wa Katiba," alisema.

# Waziri aeleza ruti za ATCL

NAIBU Waziri wa Ujenzi , Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, amesema hadi sasa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) linasafirisha abiria katika mikoa tisa nchini na nchi tano za nje.

Hata hivyo, amesema huduma za usafiri wa anga katika kila mkoa wenye kiwanja cha ndege na nchi jirani unatekelezwa kwa kufuata mpango wa upanuzi wa safari za ATCL.

Nditiye aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Khadija Nassir Ali, ambaye alitaka kujua serikali ina mpango gani katika kuhakikisha kuwa ndege za shirika hilo linafika kila mkoa hapa nchini na nchi za jirani.

Akijibu swali hilo, Nditiye alisema serikali inatekeleza upanuzi wa mtandao wa huduma za usafiri wa anga katika kila mkoa wenye kiwanja na nchi jirani unatekelezwa kwa kufuata Mpango Mkakati wa ATCL wa miaka mitano unaoishia mwaka 2021/22 pamoja na mpango wa biashara unaoandaliwa kila mwaka.

Alisema hadi sasa ATCL inatoa huduma za usafiri wa anga kwa mikoa ya Dodoma , Mwanza, Kagera, Kigoma, Mbeya, Kilimanjaro, Zanzibar, Tabora na Mtwara.

Aliongeza kuwa ATCL inatoa huduma za usafiri wa anga kwa safari za kikanda kwenye nchi za jirani ikiwamo Hahaya (Comoro), Harare (Zimbabwe), Bunjumbura (Burundi), Entebbe (Uganda) na Lusaka (Zambia).

Alisisitiza kuwa ATCL inatarajia kupokea ndege mpya zingine mbili aina ya Bombarder D8 Q400 na Boeing B787-8 mwishoni mwa mwaka huu.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Halima Bulembo, alisema gharama zinazotozwa ni kubwa, na kuhoji serikali ina mpango gani kuhakikisha zinapungua ili kila mwananchi wa kawaida aweze kumudu.

Akijibu swali hilo, Nditiye alisema ushushaji bei wa ndege hizo utategemeana na ushindani wa soko.

Naye, Mbunge wa Nyang'wale (CCM), Hussein Amar, alihoji ni kwanini wenza wa wabunge hawaruhusiwi kupita kwenye mageti ya watu maalum (VIP) kwenye usafiri wa ndege na meli.

Nditiye akijibu swali hilo alisema wenza wa wabunge wana uwezo wa kutumia VIP hivyo kama changamoto hiyo imetokea wanaomba radhi.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Tanzania sasa kuridhia biashara huru Afrika

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

TANZANIA ipo kwenye hatua za kuridhia biashara huru kwa wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) unaoundwa na nchi 55.

Akizungumza jana jijini hapa, Afisa Biashara, Thomas Mcharo, ambaye ni Mwakilishi wa Mkurugenzi Msaidizi Idara ya mtangamano wa biashara Wizara ya Viwanda na Biashara, alieleza kuwa lengo la kuanzishwa biashara ya pamoja kwa jumuiya hizo ni kukuza uchumi . Alisema biashara hiyo imegawanyika katika hatua tatu, ambayo ni asilimia 90 ya bidhaa zinazopatikana kwa wanachama wa jumuiya hiyo kutotozwa ushuru katika vituo vya forodha, asilimia tatu watalipia kwa awamu na asilimia saba hazitofunguliwa.

Mcharo alisema biashara huru itaisaidia Tanzania kutokana na mkakati wake za kuingia katika uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda, kwa kuwa viwanda vitazalisha na masoko ya kutosha.

"Awali tulikuwa tukitegemea soko la EAC na SADC, ila kuwapo kwa makubaliano haya ya Umoja wa Afrika tutajinufaisha zaidi kiuchumi, kutokana na uzalishaji wa bidhaa kuongezeka pamoja na kutanuka kwa soko," alisema.

Mtaalamu wa bidhaa na biashara kutoka Kamisheni ya Umoja wa Afrika ( AUC), Dk. Halima Noor, alisema kuwa kati ya nchi 55 zinazoiunda AU, ni nchi 52 zimesaini na nchi tatu hadi sasa hazijasaini mkataba wa maridhiano ya biashara huru kwa pamoja.

Aidha alisema kuwa wanaendelea kuhamasisha wanachama kujiunga ili kunufaika na mwingiliano wa kibiashara baina ya wanachama hao.

Naye Mwenyekiti wa meza ya majadiliano kutoka Uganda, Alexander Rubanga, alisema kuwa lengo hasa la kukutana ni kuwajengea uwezo wanachama wa AU, wakati wanaelekea kufungua biashara baina ya nchi hizo.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, kuhusu maendeleo ya ujenzi wa kituo cha ukaguzi wa watalii kinachojengwa wilayani humo juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Vijana wapewa mbinu za kukabili ukosefu wa ajira

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

VIJANA nchini wametakiwa kujishughulisha na masuala ya ujasiriamali ili waondokane na tatizo la ukosefu wa ajira ambalo limekuwa kubwa nchini na ulimwenguni kote.

Hayo yamesemwa jana katika mahafali ya sita ya kidato cha sita ya Shule ya Sekondari St. Mary's Duluti na Padre Peter Makao, aliyekuwa mgeni rasmi.

Alisema katika ulimwengu wa sasa ajira ni chache ukilinganisha na idadi ya watu wanaoingia katika soko la ajira.

"Hali hii inasababisha ushindani mkubwa katika soko la ajira, hivyo ni vyema vijana wengi waliopo majumbani na mitaani kuliko kukaa bila kazi yeyote, wakajihusisha na shughuli za ujasiriamali zenye heshima na staha. Pia wawe wabunifu," alisema.

Aliongeza kuwa vijana walio wengi wa sasa wanapenda kuwa huru kufanya mambo.

"Uhuru si jambo baya, lakini uhuru usiokuwa na mipaka na uwajibikaji huo sio uhuru, Lazima mtu awajibike kwa matendo yake mwenyewe," alisema.

Mkuu wa shule hiyo, Brother Essau Mlengule, aliwaambia kuwa hatua waliofikia ni kwa sababu ya bidii kubwa, nidhamu na kujituma katika masomo.

Aliwataka wakaendelee kujituma kwa kuwa na bidii na nidhamu watakaporejea nyumbani.

Alisema kuwa kuhitimu kwao katika masomo ni ishara ya kuwa wamekomaa kiakili, kiroho na kimwili na wapo tayari kuelekea hatua mpya ya maisha ya kitaaluma pamoja na maisha ya kujitegemea.

"Ninyi kama wasomi wa kidato cha sita, mnajukumu kubwa la kuwa wachangiaji wakubwa katika maendeleo ya maisha yenu binafsi, maendeleo ya familia, jumuiya zenu na hatimaye maendeleo ya taifa zima la Tanzania kwa fikra yakinifu

kwa matendo na kwa njia halali zinazokubalika na jamii ya watu walioelimika," alisema Mlengule.

Alisema kwamba mafanikio na maendeleo ya kweli hayaji kwa njia za mkato za kutokufuata taratibu za jumuiya husika wala kujichukulia maamuzi bila ruhusa ya mamlaka husika.

"Bali kwa kufanya kazi kwa bidii na kwa malengo, kujiamini, kuwa weledi katika kazi zenu, elimu ya fedha pamoja na kuwa na nidhamu ya fedha," aliongeza.

Alisema elimu waliyoipata iwasaidie kuwa na ujasiri wa kuishi kwa mifano ya maisha ya uadilifu katika familia na jumuiya. Pia elimu waliyoipata iwasaidie kuepukana na uvivu, ulevi, uzushi, kiburi, wizi, matumizi ya dawa za kulevya, uasherati na matendo mengine maovu yasiyokubalika katika jamii.

Alitaja baadhi ya changamoto zinazokabili shule hiyo ni upungufu wa mabweni, ukosefu wa jengo la utawala na viwanja vya michezo.

# Wito wa Nabii kulinda amani

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WATANZANIA wametakiwa kudumisha amani na upendo uliopo nchini na kuilinda kama mboni ya jicho, ikiwa njia pekee walioachiwa na Mwenyezi Mungu.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Nabii Mkuu wa Kanisa la Ngurumo ya Upako, Geordave Kisambale, wakati akizungumza na waumini wa kanisa hilo katika ibada ya Chuo cha unabii iliofanyika Kisongo nje kidogo ya mji.

Alisema Watanzania wanayo amani ambayo wamezawadiwa na Mungu, hivyo ni wajibu wa kila mtu kuienzi, kuidumisha na kuilinda.

"Unajua Mungu anatupendelea Watanzania, ametupa amani ya nchi yetu, ametufanya tunaishi kwa upendo. Angalieni nchi zingine wanapigana kila siku, kuna vita ya ndugu kwa ndugu hawapendani," alisema na kuendelea:

"Lakini sisi Watanzania tunaishi kwa amani, hivyo ni vyema amani hii tuliopewa tuilinde kama vile mboni ya jicho letu."

Aidha aliwataka Watanzania kutoruhusu mtu yeyote kuingilia amani hiyo na kuivuruga kwa kuwa hiyo ni zawadi ya pekee iliyotoka kwa Mungu.

Pia, alimtaka kila mwananchi kuendelea kuiombea nchi na viongozi wake akiwamo Rais John Magufuli, ili iendelee kuwa na amani.

"Rais anahitaji maombi kwa sababu kila siku anapigana vita vipya vya kuhakikisha wananchi wanaishi maisha safi, hivyo katika hili lazima anakutana na vikwazo na maombi ndio njia pekee ya kumlinda na kumpa nguvu," alisema zaidi.

Aidha, aliwataka Watanzania kutii sheria za nchi bila shuruti, huku akisisitiza wanasiasa kutopandikiza chuki miongoni mwa wananchi, badala yake wawaunganishe na kuwafanya kitu kimoja.







Mbunge wa Jimbo la Ndanda, Cecil Mwambe, akiwahutubia wakazi wa Kijiji cha Mbaju wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara jana, katika mkutano wa hadhara baada ya wananchi kuazimia kutoshiriki kwenye shughuli yeyote ya kimaendeleo katika kijiji chao hadi pale serikali itakapo wapelekea huduma ya umeme wa REA. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Mbinu kupunguza shehena bandarini

**Mary Mosha na Cynthia** MWILOLEZI

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Mkoa wa Tanga, imeanza mchakato wa ujenzi wa bandari kavu wilayani Arumeru mkoani Arusha itakayosaidia mikoa ya Kanda ya Kaskazini kubeba shehena ya mizigo tani 120,000 kwa kutumia usafiri wa reli unaoimarishwa kwa sasa.

Meneja wa Bandari ya Tanga, Perciaval Salama, aliyasema hayo katika mkutano maalum uliofanyika mkoani Kilimanjaro ukiwahusisha wanahabari kutoka mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Alisema ujenzi huo wa bandari kavu utawasaidia wafanyabiashara kusafirisha mizigo yao kwa wakati na kwa gharama nafuu kwa kuwa mipango yote itafanyika katika bandari hiyo kavu.

"Tunawaomba wanahabari kuelimisha jamii kutumia Bandari ya Tanga katika kusafirisha mizigo yao na kwa usalama zaidi kwani kwa sasa bandari ina jumla ya mitambo 42, na mwaka 2018/2019 imeagiza mashine 20. Kati yake, 16 sawa na asilimia 80, zimekwishawasili," Meneja Salama alisema.

Alisema mbali na ubora wa huduma zinazotolewa, pia wametoa mafunzo maalum kwa watendaji wao katika kutoa huduma kwa mteja na uaminifu.

"Katika Mkoa wa Tanga tunakabiliwa na changamoto ya bandari bubu 48, lakini tumewaelimisha wafanyabiashara, wananchi na tunatumia vyombo vya ulinzi na usalama katika harakati za kukomeza bandari hizo," alisema.

Alisema bandari yao inahudumia nchi saba za Zambia, DRC Congo, Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya, hivyo ni lazima ihakikishe inafanya kazi kwa kutumia utaalamu mkubwa wa Tehama.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Aisha Amour, aliwataka wanahabari kuitangaza bandari hiyo ili wafanyabiashara waitumie na kuachana na Bandari ya Mombasa.

# Ataka wananchi washiriki utekelezaji wa miradi

**Na Paul William,** SIHA.

UONGOZI wa Halmashauri ya Siha mkoani Kilimanjaro, umewataka wananchi kujitolea nguvu kazi ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo inayofanywa na serikali.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Valerian Juwal, alitoa rai hiyo alipotembelea Shule ya Sekondari Karansi kukagua ujenzi wa bweni kwa wanafunzi wa kike ambao kwa sasa umesimama kutokana na wananchi kugoma kujitolea kujaza vifusi vya udongo kwenye msingi wa bweni hilo. Juwal alisema serikali imetoa Sh. milioni 75 kwa ajili ya ujenzi wa bweni hilo, lakini amesikitishwa na kitendo cha wananchi wa vijiji vya Ndinyika, Kandashi na Lekirumuni kugoma kujitolea kujaza vifusi.

Alidai amepata taarifa kuwa wananchi hao wameamua kugomea mradi huo wakishinikiza Kata ya Karansi kugawanywa ili wapate kata yao.

"Inasikitisha sana kuona ujenzi wa bweni la wanafunzi kwa sasa umesimama, na hii ni kutokana na wananchi kugomea kujitolea nguvu kazi zao kujaza vifusi vya udongo, tunapaswa kutambua kuwa kukamilika kwa majengo haya kutaondoa adha kwa watoto wetu katika kupata elimu," alisema. Mkurugenzi huyo aliwataka wanasiasa wanaowatumia wananchi kufanikisha mipango yao ya kisiasa, kuacha tabia hiyo kwa kuwa si ya uzalendo, akieleza kuwa hata wananchi wanapaswa kutambua kwamba mwenye mamlaka ya kugawa kata ni Rais na si mtu mwingine.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Karansi, Erasmus Lilanga, alisema wako wanafunzi wanaosoma katika shule hiyo ambao hulazimika kutembea umbali mrefu wa kilomita 13 wakitokea mpakani mwa Wilaya za Arumeru na Siha.

Lilanga alisema kutokana na changamoto hiyo, baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakikatisha masomo yao huku changamoto ya utoro ikiongezeka kwa kasi shuleni kwake.

Anaamini kukamilika kwa ujenzi wa bweni hilo kutasaidia kupunguza changamoto hizo.

# Wadaiwa sugu bili za maji kufikishwa kortini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAMLAKA ya Bonde la Maji Mto Pangani Kanda ya Kaskazini, imesema inakusudia kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wa bili za maji na waliochimba visima bila vibali.

Vilevile, mamlaka hiyo imesema inatoa ushauri wa kitaalamu ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na uchimbaji holela wa visima vya maji.

Imesema inatoa ushauri huo wa kitaalamu ili kuepusha madhara kwa watumiaji wa visima kupata maji yasiyo salama.

Ofisa Maji Mfawidhi wa Bonde la Pangani, Sengule Sengule, aliyasema hayo jana alipozungumzia changamoto ya baadhi ya taasisi kutolipa bili za maji na kuchimba visima bila kibali.

"Kutokana na tatizo hilo, mamlaka ina kusudio la kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wote kwa mujibu wa sheria," alisema.

"Pia wataalamu wapo katika kila mkoa na wananchi wanapaswa kuwatafuta na kuwatumia ipasavyo katika kufanya utafiti wa maeneo ya kuchimba visima ili tulete mabadiliko chanya kwenye jamii.

"Kuna baadhi ya wateja wetu wakubwa kutoka kwenye kampuni na taasisi ambao wamekuwa wakikwepa kulipa bili za maji kwa zaidi ya miaka mitano na kuendelea, na tumewafuatilia, lakini bado wamekaa kimya, sasa sisi kama mamlaka ambayo inawasimamia wateja hao, tumefikia hatua za kufuata sheria."

Alisema wadaiwa sugu wote wanapaswa kutimiza wajibu wao kwa kufuata sheria na kulipa madeni hayo kwa haraka, kwa kuwa si tu watapelekwa mahakamani, bali hatua zaidi zitachukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kukatiwa huduma za maji.

"Kwa sababu hizi sheria hatutungi sisi, zimetungwa na Bunge ambalo ni wawakilishi wa wananchi kwa maslahi mapana ya nchi, kazi yetu ni kuzifuata sheria hizo," alisema.

"Tupo kwenye zoezi la kuchunguza utoaji wa vibali vya uchimbaji wa visima na zoezi hili tayari limeshaanza Tanga na baadaye Kilimanjaro, ila nawaasa tu waliojichimbia visima bila kibali, wafike wenye kwenye ofisi za mamlaka, wasisubiri adhabu," alisema.

ama
ALHAMISI APRILI 25, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 20

**Aliyezirai miaka 27 azinduka mzima**



Ukurasa 16

Mashine ya kipekee Afrika nzima kutibu kansa yaletwa



Ukurasa 15

**TB ilivyosimamiwa, UN inavyoagiza mwelekeo**



MJUE PROFESA KAISI WA SASA

# Anaambatanisha ubingwa wake hospitalini, imani kuuwezesha ujauzito ulioshindikana

Ukurasa 18

## Asiyesikia sauti yake hatimaye imekuwa

**London,** Uingereza

MSICHANA mwenye umri wa miaka saba, Leia Armitagea, aliyeishi kwa ukimya miaka miwili ya mwanzo ya maisha yake, hivi karibuni amefanyiwa upasuaji wa ubongo na kuwezeshwa kusikia.

Ni tukio lililobadilisha maisha yake, akasikia sauti za wazazi wake na kuwaambia anawapenda.

"Tuliambiwa kuwa unaweza kuweka bomu nyuma yake na asingeliweza kabisa kusikia sauti ya mlipuko wake," anasema baba yake aitwaye Bob Wine, ikianzia mtoto alipokuwa mchanga

Leia, anayetoka eneo la Dagenham, Mashariki mwa London, hakuwa na sikio la ndani au mshipa wa kusikia, hali iliyomfanya hata mtambo wa kawaida wa kusaidia mlemavu wa kutosikia au wa kupandikiziwa visingemsaidia lolote.

Ni matokeo ambayo hayakutarajiwa kwani wazazi walimpigania ili awe mmoja wa watoto wa kwanza nchini Uingereza kupewa kifaa kinachopandikizwa ndani ya ubongo kwa njia ya upasuaji mgumu alipokuwa ana umri wa miaka miwili.

Taasisi ya upasuaji huo ya nchini Uingereza, NHS imesema itadhamini upandikizaji huo kwa watoto wengine wasioweza kusikia wenye hali kama yake.

Inakadiriwa kuna watoto 15 kila mwaka nchini Uingereza, wanachunguzwa na kufanyiwa upasuaji wa aina hiyo.



Leia Armitagea (kulia), akiwa na furaha hospitalini, baada ya kuweza kusikia. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# Picha kamili ya kifua kikuu, ilivyo janga kwa afya ya wakimbizi



Raia wa Pakistani mwenye TB, aliyedumu miaka mitano bila ya kugundulika kuwa na ugonjwa huo, kutokana kushindwa kumudu Dola za Marekani mbili (Sh. 4,600) za usafiri kutoka kijijini kwake hadi hospitali ya serikali, mjini Tharparkar kupimwa afya. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), linautaja ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB), uko juu katika maambukizi na kuua duniani kote.

Hapo maana inakwenda mbali, kuhusisha vifo kwa watu wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (VVU), ambayo kwa ujumla wake ina sura ya 'chanda na pete.'

Taarifa ya WHO, zinasema TB ni ugonjwa unaosababisha zaidi vifo vinavyotokana na magonjwa, ambayo ni sugu dhidi ya dawa.

Kwa mujibu wa WHO, kifua kikuu bado ni ugonjwa unaoongoza kwa maambukizi na kuua takribani watu 4,500 kila mwaka, huku ikiwataabisha wengine takribani 30,000 duniani kote.

> **"Taarifa ya WHO, zinasema TB ni ugonjwa unaosababisha zaidi vifo vinavyotokana na magonjwa, ambayo ni sugu dhidi ya dawa.**

Tangu mwaka 2000 hadi mwaka jana, jitihada za dunia kutokomeza ugonjwa huo unaozuilika na kutibika, zimeokoa watu wanaokadiriwa kufikia milioni 54 na zimepunguza vifo vya TB kwa asilimia 42.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dkt Tedros Adhanos Ghebreyesus, anazikumbusha serikali, jamii zilizoathirika, mashirika ya kiraia, watoa huduma za kiafya na wadau wa kitaifa na kimataifa kuunganisha nguvu, chini ya mwavuli uitwao: "Tafuta. Tibu. Wote. TokomezaTB." kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma.

"Tunasisitiza umuhimu wa kutafsiri ahadi tulizojiwekea mwaka 2018 katika mkutano wa ngazi za juu wa Umoja wa Mataifa katika matendo, ili kuhakikisha kila anayehitaji huduma ya tiba ya TB anapata," anasema Dk. Ghebreyesus



Dk. Robert Koch, mtaalamu aliyegudua bakteria wa TB.

Hivi karibuni, WHO ilitoa mwongozo mpya wa kuboresha namna ya kutibu kifua kikuu sugu kwa dawa na imetoa ushauri unaohusisha haja ya sekta mbalimbali kufuatilia ugonjwa huo.

Mkuu huyo wa WHO anaeleza haja ya kufanyika mapitio ya maendeleo na hatua, kuweka kipaumbele cha mipango na utekelezaji wa kupambana na TB na kikosi kazi kinachohakikisha ushiriki wenye tija wa jumuiya za kiraia.

**WAHAMIAJI HATARINI**

Kutokana na TB kuwa ugonjwa wa kuambukiza na kwa njia ya hewa, jamii ya wahamiaji imo katika makundi yaliyoko hatarini zaidi, kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Wahamiaji (IOM).

Shirika hilo linasema wahamiaji wengi wanafanya kazi katika mazingira hatari, kazi ngumu na wanaishi katika makazi yaliyo na kiwango cha chini, pia baadhi wako kwenye vizuizi au kambi za wakimbizi zenye idadi kubwa ya wakazi.

Pia, IOM inasema wahamiaji wanakumbana na changamoto za kikwazo cha lugha, uongozi na hata utamaduni katika kuzifikia huduma za kiafya na mara nyingi wanaondolewa katika mfumo wa ulinzi wa kijamii na programu za bima ya afya kwa wote.

Wakati kila Machi 24 ya mwaka ni maadhimisho ya Siku ya TB, IOM ina maoni kuhusu ugonjwa huo na athari zake kwa afya ya jamii, pia mtazamo wa kiuchumi na hatua stahiki za kuchukuliwa kuutokomeza duniani kote.

Siku ya TB ni maalum kwa kumbukumbu ya siku ambayo, mwaka 1882, mtaalamu Dk. Robert Koch alitangaza kugundua bakteria anayesababisha TB na hivyo ikafungua njia kuelekea kuugundua ugonjwa na matibabu yake.

AFYA

# TB ilivyosimamiwa nchini, UN inavyoagiza mwelekeo

- Unaijua 'Tanzania Stop TB Partnership'?
- Wagonjwa wapya, sugu waibuliwa kwa kasi

Na Yasmine Protace

***ALHAMISI iliyopita, jarida hili lilikuwa na makala inayohusu ugonjwa wa kifua kikuu nchini na sura yake kimataifa, ikiegemea nafasi yake kijinsia. Leo ni mwendelezo wa ufafanuzi wa ugonjwa huo, ambao maadhimisho yake ya mwaka yalikuwa mwezi uliopita.***



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kushoto), akishiriki ugawaji dawa za TB, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

UGONJWA wa kifua kikuu (TB), upo katika nafasi ya tisa, katika orodha ya magonjwa ya kuambukiza yanayosababisha vifo duniani kote.

Nchini inaelezwa TB inaongoza katika kusababisha vifo vingi miongoni mwa magonjwa ya kuambukiza, ikifuatiwa na Ukimwi.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema TB inasababisha wastani wa vifo 70 kwa siku, ambavyo ni sawa na vifo watu 3 kwa saa, njia kuu ya uambukizaji inatajwa kupitia hewa.

Taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), inasema TB huathiri takriban watu milioni 10.4 duniani kila mwaka na asilimia 25 wanatoka barani Afrika.

Katika janga hilo, Tanzania imo katika nchi za Afrika zenye kiwango kikubwa cha wanaougua TB, ikikadiriwa kuna jumla ya wagonjwa wapya 154,000 kila mwaka.

Waziri anasema mwaka 2017 Tanzania iligundua na kuwapatia matibabu takribani wagonjwa 75,000, ambayo ni asilimia 44 ya wagonjwa wanaokadiriwa wapya wa TB.

"Hii ina maana ya kuwa wagojwa 85,000 hawagunduliwi, hivyo kukosa matibabu kila mwaka nchini Tanzania," anasema Waziri Ummy na kuongeza:

"Hii ndiyo changamoto kubwa iliyo mbele yetu na tunawajibika kuwafikia, kuwaibua na kuwaweka katika matibabu wagonjwa wote wa TB. Kama nchi, pia tumekuwa na tatizo la kuwafikia na kuwagundua wagonjwa wote wa kifua kikuu sugu."

Takwimu za mwaka 2017, zinaonyesha kuwapo wagonjwa sugu 443 wa TB waligunduliwa na kuanzishiwa matibabu, kati ya 1,700 wanaokadiriwa kuwapo.

Waziri Ummy anaongeza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP), inaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Miaka Mitano (2015-2020).

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, lengo lililopo ni kupunguza nchini kote, maambukizi mapya ya TB kwa asilimia 20 na idadi ya vifo vinavyotokana na TB kwa asilimia 35, ifikapo mwaka 2020.

> **"Hii ina maana ya kuwa wagojwa 85,000 hawagunduliwi, hivyo kukosa matibabu kila mwaka nchini Tanzania.**

Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, nayo inaendelea kuhudumia uchunguzi na matibabu bila ya malipo katika vituo vya kutoa huduma vya serikali na binafsi.

Waziri anasema, utekelezaji huo ndio uliowezesha kuwafikia wagonjwa 75,845 ambayo imevuka malengo ya mwaka jana, ikiwa ni ongezeko la asilimia 22 kutoka mwaka 2015, mpango mkakati ulipoanza.

Anasema katika sura nyingine, ndani ya kipindi hicho cha utekelezaji malengo, kuna ongezeko la asilimia 153 kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu kutoka 176 wa mwaka 2015, hadi 449 mwaka jana. Waziri Ummy anasema, pamoja na ukubwa wa tatizo la TB duniani, bado jitihada hazitoshelezi kukidhi haja ya mapambano na utokomezaji wa ugonjwa huo, hali iliyoifanya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kukutana mwezi Septemba mwaka jana, kutafakari suala hilo.

Anasema, walifikia hatua ya mara ya kwanza kuweka maazimio na malengo ya kuongeza kasi ya kutokomeza TB duniani, ifikapo mwaka 2030.

### MAAGIZO YA UN

"Baraza Kuu limezitaka nchi wanachama kubadilisha mapambano ya TB kuwa ya sekta zote, badala ya sekta za afya pekee. Vilevile, limeweka malengo kwa nchi zote ambazo zina tatizo kubwa la TB.

"Tanzania tunawajibika kuwagundua na kuwaweka katika matibabu ya TB wagonjwa 97,200 wa TB kwa mwaka huu 2019 na kiasi cha wagonjwa 139,000 kwa mwaka 2020," anasema.

Anaongeza kuwa malengo makubwa yanahitajika katika kujipanga sawa, akieleza imani yake katika kufanya kazi kwa pamoja na kushirikiana, katika kukidhi haja hiyo.

Ummy anasema, ili kwenda sambamba na maazimio ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, wizara inaanzisha muungano wa wadau mbali wa asasi za kiraia na kijamii utakaojulikana kama 'Tanzania Stop TB Partnership.'

Anaainisha kuwa, ni muungano wa kitaifa utakaowaleta pamoja washirika kutoka sekta mbalimbali, kuongeza kasi ya kutekeleza mipango ya pamoja ya kutokomeza TB nchini.

"Natarajia kuwa muungano, huu wa wadau wa sekta mbalimbali, utaongeza chachu kwa kuchangia rasilimali fedha, mali au ujuzi walio nao," anasema na kuutambulisha kuwa ni chombo kilichoanzishwa kimataifa mwaka 2001.

Kwa mujibu wa Ummy, chombo hichi msingi wake ni mkakati wa kupambana na TB na makao makuu yake yapo jijini Geneva, Uswisi. Hivi sasa kuna mashirika takriban 1,500 duniani kote, yakijumuisha serikali, taasisi za utafiti, mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kiraia, vikundi vya kijamii na sekta binafsi.

Ummy anasema 'Stop TB Partnership' umeshaundwa katika nchi 27 duniani kote, kati yake, saba zinatoka barani Afrika; Kenya, Uganda, Nigeria, Swaziland, Sudan, Msumbiji na Ghana, uzoefu unaonyesha kuwa chachu ya mafanikio.

Anawataja wadau wakuu waliochangia kuanzishwa chombo hicho nchini, ni Shirika la Misaada la Marekani, kupitia taasisi za KNCV na Global Fund na Health Promotion Tanzania (HDT).

AFYA

# Mashine ya kipekee Afrika nzima kutibu kansa yaletwa nchini kukabili ongezeko

• Imeokoa bajeti mil. 50 mgonjwa kwenda India • Samia: Wageni kumiminika kwetu kutibiwa • Ummy ataja maeneo kansa ilikojikita

**Na Mary Geofrey**

SARATANI ni ugonjwa usioambukiza, lakini hatari na idadi ya wagonjwa inaendelea kuongezeka kwa kasi kila mwaka nchini na duniani kote.

Ripoti ya mwezi Septemba mwaka jana, iliyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Utafiti wa Saratani (IARC), onaonyesha nchini Tanzania kunakadiriwa kuwapo wagonjwa wapya 42,060 na takribani wagonjwa 28,610 hufariki kwa mwaka.

Inaelezwa, kama juhudi za kinga na tiba hazitaimarishwa, hadi kufika mwaka 2035 katika nchi hizo, vifo vitokanavyo na saratani vinatarajiwa kuongezeka kufikia milioni 24 duniani kote kila mwaka.

Tayari serikali imeshachukua hatua stahiki kutokana na kushamiri kwa ugonjwa huo nchini. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeshatoa Sh. bilioni 9.5, kwa ajili ya kununua mashine za kisasa kutibu wanaougua saratani.

Mashine hizo hizo za kisasa zinazotambulika kwa jina la 'CT Simulator' na mashine mbili za tiba ya mionzi kwa teknolojia ya kisasa aina ya 'Linear Accelerator.'

Waziri mwenye dhamana, Ummy Mwalimu, anasema katika uzinduzi wa mashine hizo, zilizoanza kazi miezi sita iliyopita katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, anasema zitasaidia kuokoa fedha za serikali zilizotumika kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kutibiwa.

"Mashine hizi zitasaidia kuokoa fedha nyingi ambazo zilikuwa zinatumiwa na serikali kupeleka wagonjwa kwenda nje ya nchi na kwa mwaka, zilikuwa zinatumia Sh. bilioni 7.5," anasema Ummy na kwamba zimesaidia kupunguza muda wa wagonjwa kumulikwa mionzi kutoka wiki sita hadi tatu.

"Kwa mwaka jumla ya wagonjwa 300 walikuwa wanaenda rufaa nje ya nchi, hasa India, kwa ajili ya kupata tiba. Mgonjwa mmoja hugharimu Sh. milioni 50, ikiwamo tiba ya mionzi, malazi na usafiri," anaeleza zaidi Ummy.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage, akitoa maelezo kwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuhusu ufanisi wa mashine mpya. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### KULIVYO NCHINI

Waziri Ummy anasema, hali ya nchi kupitia takwimu za Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, inaonyesha saratani zinazoongoza ni ya: Mlango wa kizazi kwa asilimia 31; ikifuatiwa na matiti kwa asilimia 31; kansa ya kooni na njia ya chakula, kwa asilimia 10; na 'kaposi sakoma' kwa asilimia tisa. Hiyo ni kansa inayoanza kwa sehemu ya chembe hai na inakua. kisha inajiumba kuwa kansa.

"Kama inavyoonekana saratani ya matiti inaongezeka sana na kuwa ya pili, wakati miaka ya nyuma ilikuwa ya tatu. Vilevile saratani ya koo njia ya chakula, imekuwa ya tatu, wakati kwa miaka kadhaa ilikua ya nne. Kwa ujumla, saratani zote zinaongezeka nchini kwa sababu mbalimbali," anasema Ummy.

> **Kwa kweli nilisikitika sana kipindi hicho, kwa sababu wagonjwa wa saratani walikuwa na malalamiko mengi sana.**



Waziri Ummy akimsikiliza ndugu wa wagonjwa waliofika hospitalini mwaka jana.

### KWA NINI HIVYO?

Waziri Ummy anataja sababu za kuenea kwa ugonjwa huo, ni kuongezeka umri wa kuishi kila mwaka kutokana na mikakati ya kuboresha uchumi na kuimarika kinga na matibabu ya magonjwa ya kuambukiza.

"Saratani ni ugonjwa unaoendana sana na kuongezeka umri. Miaka 15 hadi 20 iliyopita, makadirio ya umri wa kuishi ilikuwa miaka 48, lakini takwimu za hivi karibuni zinaonyesha umri wa wastani wa kuishi ni miaka 63," anasema Ummy.

Waziri pia anaeleza, kuwapo mabadiliko katika mfumo wa maisha ya umma, kunakosababisha saratani na magonjwa mengine yasiyoambukiza.

Anataja visababishi hivyo ni matumizi ya tumbaku, unwyaji pombe kupita kiasi, ulaji vyakula usiofaa, kutofanya mazoezi kila mara, kuweka mwili katika afya na kupunguza uzito.

Ummy anataja sababu nyingine ni kuongezeka kwa mwamko wa jamii katika utumiaji wa huduma za afya na ubora wa vipimo na anafafanua: "Hii inafanya wagonjwa wengi kufika hospitali ambapo wanagundulika kwa haraka tofauti na miaka ya zamani."

Anarejea mwaka 2015 wakati awamu iliyopo ya kiserikali ilipoingia madarakani, kulikuwapo wagonjwa wapya 8,200 tu waliohudumiwa hospitalini, ambao ni asilimia 19.6 ya wagonjwa wote nchini.

Ummy anasema wakati, zilikuwa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road jijini Dar es Salaam na Hospitali ya Bugando, iliyoko Mwanza, ndizo zilitibu wagonjwa wa saratani.

"Baada ya kuimarisha huduma za saratani katika kipindi cha miaka miwili tu, wagonjwa wapya wa saratani 13,400 wanahudumiwa kwa mwaka katika hospitali za Ocean Road, Bugando, Muhimbili, KCMC (Moshi) na za binafsi sawa na asilimia 31.9 ya wagonjwa wote wa saratani nchini," anaeleza Ummy.

Anasema, takwimu hizo zinatoa tafsiri kwamba, wagonjwa wengine walishindwa kufika hospitali kwa sababu mbalimbali, ikiwamo umbali mrefu kufika hospitalini kunakopatikana huduma hiyo.

Kiongozi huyo anasema, hata wagonjwa waliofika hospitalini walikutana na changamoto za kukosekana dawa, kusubiri muda, kukosa tiba na msongamano wa wagonjwa wodini na sasa kuna maboresho.

"Tunamshukuru sana Rais John Magufuli kutupatia fedha za kuimarisha huduma za saratani nchini. Tumeona jinsi zilivyoboreshwa na ndiyo maana hata wagonjwa wanafika kwa kiwango kikubwa," anasema Ummy.

## Mambo 10 ya kukabili saratani

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), mwaka jana lilisema saratani ni chanzo cha kifo kwa wastani wa kila mtu mmoja, kati ya sita walioko duniani.

Wakati kuna hali hiyo, nusu ya aina zote za saratani zilizoko duniani, zinazuilika.

Hata hivyo, ikirejewa katika uhalisia ni kwamba, kuna matukio mapya ya ugonjwa huo yanayongezeka kwa takriban asilimia 70 katika miongo miwili ijayo.

Utumiaji tumbaku ndio hatari kuu ya chanzo cha kuugua saratani na ndio chanzo cha takriban asilimia 22 ya vifo vinavyotokana na saratani na WHO inaitaja saratani ya matiti inaongezeka, hususan katika mataifa yanayoendelea.


Kuna mambo 10 yanayosaidia kupunguza hatari ya mtu kuugua saratani:

- Usivute sigara, wala kutumia tumbaku ya aina yoyote.
- Hakikisha nyumbani kwako hamna moshi
- Kula chakula chenye afya.
- Kunyonyesha kunapunguza hatari kwa mama kuugua saratani
- Hakikisha watoto wako wanapata chanjo dhidi ya hepatatis B na HPV:Homa ya Hepatitis B hutokana na kirusi kinachoambukizwa kupitia damu na majimaji mengine ya mwili na huivamia ini na kusababisha vifo na HPV ni virusi vinavyopatikana na kuwepo maji maji mwilini, kutokana na ngono.
- Epuka kuchomwa sana na miale ya jua, au tumia mafuta yanayokinga dhidi ya miale hiyo, hasa kwa watu weupe.
- Punguza uchafuzi wa hewa ndani na nje ya nyumba
- Jishughulishe kuupa mwili mazoezi
- Punguza unywaji wa pombe
- Jitahidi kufanyiwa ukaguzi wa mapema kutambua uwepo wa saratani.

Nchini Kenya, ni ugonjwa wa pili unaochangia vifo vya watu, ukitanguliwa na moyo.

Ni wachache wanaoweza kumudu gharama kubwa katika hospitali za kibinafsi.

**Kwa mujibu wa Mtandao.**




Namna ilivyo sigara na athari zake kwa afya ya mtu. **PICHA: MTANDAO.**



Mratibu wa Afya ya Uzazi wa Mama, Vijana na Jinsia, kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Gerald Kiwele, akizungumza katika uzinduzi wa jukwaa hilo, Machi 15, mkoani Iringa. **PICHA: MARY GEOFREY.**

### MCHAKATO ULIPOANZIA

Ummy anaeleza alipoteuliwa kuongoza wizara hiyo, alifanya ziara ya kwanza katika taasisi hiyo kuzindua Bodi ya Wadhamini na alizunguka kuangalia hali ya utoaji huduma.

"Kwa kweli nilisikitika sana kipindi hicho, kwa sababu wagonjwa wa saratani walikuwa na malalamiko mengi sana," anasimulia Waziri Ummy, akiendelea:

"Kuna mgonjwa aliponiona katika wodi akawa ananikimbilia kunililia wakati akiwa na dripu ambayo ikachomoka na kuanza kuvuja damu. Hali ilikuwa mbaya sana."

Anasema kutokana na hilo, aliiagiza bodi ya wadhamini na menejimenti, kuboresha huduma na akaahidi kuongeza upatikanaji wa dawa za saratani.

Waziri anaeleza hatua mojwapo iliyochukuliwa ni kuongeza bajeti ya tiba ya saratani, kutoka Sh.milioni 790 katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi Sh. bilioni saba, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17.

"Na kwa miaka yote iliyofuata bajeti ya Sh. bilioni saba kwa mwaka imekuwa inawekwa kwa dawa za saratani kwa taasisi hii na kuanzia mwaka huu fedha zimetengwa pia kwa ajili ya Hospitali ya Bugando na KCMC," anaeleza.

> **Kuna mgonjwa aliponiona katika wodi akawa ananikimbilia kunililia wakati akiwa na dripu ambayo ikachomoka na kuanza kuvuja damu. Hali ilikuwa mbaya sana.**

### MAFANIKIO

Makamu wa Rais, Samia Hassan, aliyekuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa mashine hizo, anasema hazijawahi kuwapo katika nchi za Afrika na kwamba zitawasaidia wananchi kupata fedha za kuendesha hospitali hiyo.

"Kuwapo kwa mashine hizi za kisasa nchini ambazo hazipo Afrika, zitawezesha wagonjwa wa sekta binafsi kufuata huduma hii na wanaotoka nje ya nchi kuja nchini kufuata matibabu yatakayowezesha kupata fedha zitakazosaidia taasisi kujiendesha na kununua mashine nyingine kama hizi," anasema Samia.

Anausihi uongozi wa taasisi hiyo, kuitangaza huduma hiyo nchi nyingine, ili wagonjwa waliokuwa wanapelekwa India na nchi nyingine duniani waletwe nchini kupata matibabu kwa gharama zao.

"Wagonjwa wa nchi nyingine waletwe kupata matibabu ya kulipitia na si bila malipo kama sera ya nchi yetu inavyosema matibabu bila malipo kwa Watanzania tu. Msiwatoze gharama kubwa za kuwakomoa, bali zile zinazotakiwa kutuingizia mapato," anasema Samia.

Pia, anasema fedha zitakazopatikana kutoka kwa wagonjwa binafsi na wanaotoka nje ya nchi, zitawezesha kununua mashine kama, zitakazofungwa katika hospitali za kanda na mikoa nchini.

Samia, pia anaahidi serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa vifaa vya kisasa vya matibabu, ili kuwapunguzia wananchi mzigo wa kufuata huduma nje ya nchi.

### MKURUGENZI OCEAN ROAD

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage, anasema awali serikali ilitenga Sh.bilioni 14 za kununua mashine hizo za kisasa kupitia wakala, lakini wakaagiza moja kwa moja kutoka kiwandani kwa bei ya Sh. bilioni 9.5, hivyo imeokoa sh. bilioni 4.5.

Anasema gharama za ujenzi wa jengo na ununuzi wa mashine hizo umefanyika kwa fedha za serikali kwa asilimia 100.

AFYA

## MJUE PROFESA KAISI WA SASA

# Anaambatanisha ubingwa wake hospitalini, imani katika tiba

- Ajisifu wengi waliomfuata kwake 'imewezekana'
- Akataa malipo, aelekeza marejesho kwa Muumba
- Mstaafu mgonjwa, anayeota kumalizia alichobuni

**Na Beatrice Moses**

***KATIKA mfululizo wa makala mbili zilizopita, zilimueleza Profesa Malise Kaisi na maudhui mengi aliyoyatenda kuhusu afya ya kinamama na uzazi. Je, kwa sasa anafanya nini na yepi maoni yake. Endelea kumfuatilia.***

Ni mzee wa umri miaka 76 sasa. Yupo makini muda wote. Hata unapomwangalia usoni, wajihi wake ni nadra kubeba tabasamu, hasa anapokuwa kwenye mazungumzo anayoyapa umuhimu. Hiyo ndio hulka yake ya sasa.

Muundo wa umbile lake ni kubwa kwa wastani, ikibebwa na urefu, huku kichwani kwake kuna nywele zenye rangi mbili, nyeusi ya asili iliyopambwa na mvi.

Huyu ni mtaalamu wa afya na daktari bingwa wa uzazi na magonjwa ya wanawake, Profesa Malise Kaisi. Nipashe ilimtembelea nyumbani kwake, jijini Dar es Salaam siku kadhaa zilizopita, akitaka kujua mengi kuhusiana na kazi.

Mtazamo unajikita katika maisha yake ya sasa; pia zama za ustaafu wake, kwani sifa zake ziko wazi ni maarufu sana nchini. Baada ya salamu, ghafla nilijikuta nimezama zaidi kwenye mawazo kuhusiana na alivyo nayo sasa, akiugua maradhi ya kiharusi na jinsi alivyojikita katika kusoma na kuandika vitabu.

Hata hivyo, nakiri si mara yangu ya kwanza kumtembelea. Mara zote ninapofika hukuta ana mgeni au wageni, ambapo wengine hufika kwa ajili ya kuomba ushauri wa kitabibu, baadhi wanafika kumsalimia.

Profesa Kaisi, alifundisha katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na hata awali kilipokuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Udaktari.

Ni vigumu kupata idadi ya wagonjwa ambao amewahi kuwahudumia, lakini ni wazi wanawake na wanaume aliowahi kuwatibu au kuwashauri, wanatambua ubora wa huduma yake.

Kutokana na maradhi aliyonayo sasa, hawezi tena kushika mkasi kuingia kwenye chumba cha upasuaji, licha ya kwamba bado ana uwezo mzuri wa kutoa elimu ya kitabibu hasa ya uzazi.



Profesa Malise Kaisi.

> **Katika hilo amekuwa akishirikiana na baadhi ya wachungaji kuwafanyia maombi nao wanapokea uponyaji.**

### ALIKOTOKEA

Profesa Kaisi, ambaye asili yake ni wilayani Kyela, mkoa wa Mbeya, alihitimu kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora, kisha akajiunga na elimu ya juu kwenye Chuo Kikuu cha Makerere, nchini Uganda alikohitimu mwaka 1968.

Anasema, baada ya hapo alirudi nyumbani na kuanza kazi mwezi Aprili mwaka 1969, katika iliyokuwa Hospitali ya Muhimbili, ambayo sasa ni Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Profesa Kaisi, alihamishiwa katika Hospitali ya Mawenzi iliyoko mjini Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro mwaka 1970, kabla ya kuchaguliwa kuwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mtwara (RMO), mwaka 1971.

Wasifu wake umebaki katika historia, ambayo binafsi anakiri ya kufanya kazi kwa kujituma na ubunfu, ikiwamo kufanikiwa kutoa mafunzo ya kuhudumia wajawazito na watoto wachanga vijijini.

Anasema, baada ya hapo aliamua kujiendeleza kielimu mwaka 1973 katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba cha Muhimbili (Muhas), alikojikita katika tiba ya magonjwa ya wanawake na uzazi.

Hiyo ni kupitia andiko lake la kuomba kuanzishwa mradi wa mafunzo ya kutoa huduma za awali kwa mama na mtoto, ambalo lilifanikiwa.

### AKUMBUKA SAFARI YAKE

Profesa Kaisi anasema, katika utendaji kazi, kuna mambo yalitendeka kwa kiwango cha kumfurahisha na mengine yalimpa changamoto, akalazimika kuyafanya katika nafasi ya uzazi, kwa maana ya baba na kuweka fani yake pembeni kwa muda.

Katika hilo, anagusia linalomfurahisha, kwamba ameacha alama ya kufanikiwa kwa huduma ya mama na mtoto, huku akikumbuka changamoto ya ubishi wa baadhi ya wanaume kwenda hospitali.

Daktari huyo bingwa anataja njia aliyotumia ni kwa jina la kitaalamu, IVF, ambayo inamsaidia utungishwaji mimba kwa njia ya kupandikiza mbegu za mwanamume, ndani ya yai la mwanamke na kuwekwa kwenye tumbo la uzazi la mwanamke baada ya saa 40.

"Mara kadhaa nimejikuta nalazimika kuwa baba wa wagonjwa wangu wa kike, kwa kuwaita waume zao wakati mwingine kwa kuwabembeleza au kuwafokea, ili mradi tu kuhakikisha wanafika ili tufanikishe vipimo vinavyohitajika.

'Mimi nilikuwa nashambuliwa, watu wakidhani kuwa nitadai mamilioni ya fedha kwa huduma hiyo ya IVF. Nashukuru kwamba, sasa kuna kliniki kadhaa zimefunguliwa, hivyo inafanyika hapa nchini, ingawa kwa gharama kubwa," anasema Profesa Kaisi.

### ANAVYOMCHA MUNGU

Anasema, licha ya uhalisia wa kutoweza kutibu kwa vitendo kutokana na hali aliyo nayo kiafya, bado anaelekeza shukurani kwa Mungu, kumuwezesha kuwahudumia kwa namna ya kipekee.

"Wapo wanaoshindwa kunielewa. Lakini, hali ambayo imekuwa ikinitokea, yaani mtu anakuja hapa ananieleza matatizo yake hasa hawa ambao hawajapata watoto. Nasikia sauti ikiniambia, mwambie mwezi huu atapata mimba,"anaeleaza Profesa.

"Mara nyingi anapenda kukaa hapa (anaeleza alikokaa pichani). Pangekuwa panapingwa picha na kurekodiwa hapa, watu wangeona ninachokieleza. Mungu huwa anasema na mimi, hajawahi kuniambia uongo maana yeye ni mwaminifu," anaongeza.

Anatetea udhihirisho kuwa, asilimia kubwa ya aliowaelekeza kuwapa ujumbe huo, wamefanikiwa. Wapo wengine tayari wana watoto, wengine wajawazito.

Profesa Kaisi katika hilo, anaeleza mafanikio ya msaada wake kiimani, ambao anajumuisha na taaluma yake akisema, huwa hapendi wanaofanikiwa wampelekee shukrani, wahamishie kwa Mungu.

Katika utekelezaji wa azma hiyo, Profesa Kaisi, anabainisha kuwapo maneno ya vitisho yanayotolewa na baadhi ya madaktari kwa wagonjwa, ikiwamo kuwakatisha tamaa, pale wanapobainika kuwa na uvimbe tumboni.

"Ni kweli kwamba wanawake wengi wanasumbuliwa na uvimbe. Wakati mwingine inaweza kuondolewa baada ya muda ikabainika kuwa umejitokeza mwingine, lakini hiyo haimaanishi kwamba hawezi kushika mimba, kwa neema ya Mungu," anasema.

Bingwa huyo wa tiba ya kinamama na uzazi, anasema pia wapo kinamama wanaosumbuliwa na matatizo ya kukosa watoto, lakini anakiri katika baadhi ya mazingira, kuwapo uhusiano na nguvu za giza.

Anasema, katika hilo amekuwa akishirikiana na baadhi ya wachungaji kuwafanyia maombi nao wanapokea uponyaji.

Katika msimamo wake huo, Profesa Kaisi, anasema anapokea wagonjwa wanaotafuta ushauri kwake, bila ya kujali dini zao, huku akifafanua kwamba amekuwa akipata maono kwa wote kwa sababu ya anachokitamka: "Mungu ni wa wote na njia zake hazichunguziki."

Anasema, bado ana kiu ya kuwahudumia kinamama wanaosumbuliwa na matatizo ya uzazi, hivyo anatamani kuanzisha kliniki ya IVF

"Naamini Mungu atanipa nafasi ya kutimiza hii ndoto yangu, nitashirikiana na madaktari vijana, kutakuwa na program exchange na kliniki nyingine nitakayofanikiwa kuunganisha ushirikiano nao katika kufanikisha hili," anasema.

MAZINGIRA

# Msitu wa Pugu, mapafu ya hewa Dar yasiyojulikana kwa wengi

• Miti yake ndio iliyozaa jina Pugu • Mbioni kuwa kiota cha utalii kitaifa

Na Elizabeth Zaya

HIFADHI ya Msitu ya Pugu, ndiyo inayotegemewa kama mapafu ya jiji kubwa la kibiashara, Dar es Salaam.

Kwa kurejea faida lukuki zinazotokana na misitu, shughuli mbalimbali za uzalishaji zikiwamo za viwanda kwa jiji na maeneo jirani, misitu hiyo ndiyo inayofanya kazi kubwa kufyonza hewa chafu na kurejeshea hewa safi wakazi.

Historia ya Hifadhi hiyo ambayo ikaipa jina la Hifadhi ya Pugu, inatokana na mti aina ya Mpugupugu, unaopatikana katika hifadhi hiyo pekee, jina hilo likasambaa hadi katika Shule ya Sekondari ya Wavulana Pugu, ambayo ni kongwe.

Ofisa Misitu Mkuu na Mkuu wa Ugani na Uenezi TFS, Shabani Kiula, anasema umuhimu uliopo katika msitu huo ni mkubwa kuhakikisha unalindwa kwa nguvu zote.

Anataja sababu za haja ya kuwa na ulinzi madhubuti ni kudhibiti uvamizi na uharibifu wa aina yoyote. Kiula anafafanua: "Kwa umuhimu na faida zilizopo katika msitu huu, tunahitaji kuwekeza nguvu kubwa katika kuulinda. Tuhakikishe kwamba hakuna uvamizi wala uharibifu wowote kwa sababu."

"Kiasi kikubwa cha hewa katika jiji la Dar es Salaam, kinategemea msitu huo, pamoja na Kazimzumbwi. Sijui ingekuwaje isingekuwapo msitu huu?" anahoji na kuongeza ufafanuzi:

"Hii misitu miwili ya Kazimzumbwi na Pugu ndiyo mapafu ya Dar es Salaam. Shughuli zote za viwanda na hewa chafu inayozalishwa katika jiji hilo, inafyozwa na misitu hiyo halafu inazalisha hewa safi ya Oksijeni."

### JUHUDI YA TFS

Anasema katika muongo mmoja uliopita, misitu ya Pugu na Kazimzumbwi, ilianza kuharibiwa, kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu. Lakini kuna juhudi kubwa imefanywa na TFS kuiokoa.

"Hali ya msitu kwa sasa iko vizuri. Kazi ambayo ilifanywa kwa nguvu kubwa na TFS kuhakikisha inauokoa na kuurudisha katika hali yake na kwa sasa hali ni nzuri na wananchi wanaouzunguka wanafaidi matunda yake," anajisifu Kiula.

Anasema mbali na faida katika miji inayozunguka misitu hiyo, lakini pia inaingiza kipato kinachotokana na shughuli za kitalii.

### UNAPANDA HADHI

Meneja Masoko wa TFS, Mariam Kobelo, anasema serikali iko katika mkakati wa kuupandisha hadhi Msitu wa Hifadhi wa Pugu, kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule za Sekondari za Pugu na Minaki, wakiwa na maofisa wa TFS, walipotembelea Hifadhi ya Msitu wa Pugu, Dar es Salaam, hivi karibuni. **PICHA ZOTE: ELIZABETH ZAYA.**

> "Ukiwa chini ya msitu wa mazingira asilia utakuwa chini ya uangalizi madhubuti. Haitoruhusiwa shughuli zozote za kibinadamu kufanyika ndani ya msitu huu, isipokuwa shughuli za kitafiti, elimu na ikolojia.



Wanafunzi waliotembelea Hifadhi ya Msitu wa Pugu, Dar es Salaam.

Anasema, endapo utapandishwa katika hadhi hiyo, hautatumika tena kwa shughuli za kibinadamu, bali utajikita kwa mengine, ikiwamo utalii. Anasistiza:

"Ukiwa chini ya msitu wa mazingira asilia utakuwa chini ya uangalizi madhubuti. Haitoruhusiwa shughuli zozote za kibinadamu kufanyika ndani ya msitu huu, isipokuwa shughuli za kitafiti, elimu na ikolojia."

"Nawaambia Watanzania kwamba, wanakosa kufahamu vitu muhimu kwa kushindwa kutembelea hifadhi za misitu. Kuna faida nyingi katika misitu ambazo watu wengi hawazijui na msitu huu ndiyo 'mapafu' ya jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, ni vyema kujenga tabia ya kuitembelea, wasikariri kwamba utalii ni wanyama tu."

Hifadhi ya Msitu wa Pugu, mbali ya kuwa na vivutio vya miti adimu, vingine ni mapango ya popo, ambayo zamani yalitumika katika shughuli za uchimbaji madini.

"Ndani ya msitu hii kuna vitu vya kufurahisha, kuna mabwawa humu, tuna ndege wa kuvutia, vipepeo wa kipekee, digidigi, kuna mapango ya popo ambayo zamani yalikuwa yakitumika kuchimba madini,"anasema Mariam.

Anasema TFS imeendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali ikiwamo katika mashule, katika taasisi mbalimbali na katika makazi ya wananchi kuhusu umuhimu na faida za misitu.

"Tunaelimisha jamii faida ziliziziopo katika misitu, tunataka macho yao yafunguliwe, waone fursa za misitu, mbali na kuwa chanzo cha maji na uzalishaji wa hewa safi, pia wajifunze kufuga nyuki na fursa nyinginezo,"anasema Mariam.

Kwa mujibu wa meneja huyo, kuna shule zinazopeleka wanafunzi kujifunza msituni, namna ya kutunza mazingira na faida zake mbalimbali, lengo ni kujenga jamii yenye uelewa sahihi kuhusu misitu

"Tunafahamu wanafunzi ni kundi muhimu katika jamii, kwa sababu ndio viongozi wajao. Kwa hiyo, tukijenga uelewa kwa viongozi hawa wajao, tunaamini watakuwa mabalozi wazuri katika uhifadhi wa mazingira,"anasema Mariam.

Anaongeza kwamba. TFS imetoa fursa kwa wawekezaji kujitokeza kuchangamkia fursa ya kuwekeza katika sehemu za hifadhi misituni, kwa kujenga hoteli na kuanzisha huduma mbalimbali za jamii katika maeneo hayo.

Mariam anasema lengo ni kuhakikisha huduma zote za kijamii zinapatikana katika maeneo hayo, ili kuepusha usumbufu kwa watalii wanaokwenda kufanya utalii katika hifadhi za misitu.

"Lengo letu tunataka kuboresha pia utalii ikolojia, tunataka kuhakikisha kwamba watalii wanapokuja kufanya utalii wasihangaike kufuata mbali huduma.

"Tunataka ziwapo hoteli ambazo watalala, chakula watapata huko huko na hata huduma nyinginezo zikiwamo za fedha, ili kusiwe na sababu ya wao kulazimika kwenda mijini kufuata huduma hizo," anasema Mariam.

Pia, anautaja utalii mwingine maarufu katika msitu huo, ni kuwapo mapango ambayo yamekuwa yakitumika katika ibada.

Mariam anasisitiza kwamba katika kulinda misitu hiyo, TSF imeweka mikakati madhubuti ya kupambana na waharibifu.

AFYA

# Mama mzee asiyewahi kuhisi maumivu maishani mwake

JO Cameron (65), aligundua kuwa ngozi yake inaungua mpaka anaponusa harufu ya kuungua kwa ngozi yake. Mara nyingi mikono yake huungua kwenye jiko la kuokea, lakini hahisi maumivu ya kumpa tahadhari kuwa yuko hatarini.

Huyo ni mtu wa pili duniani mwenye hali hiyo, inayoelezwa kuwa na mabadiliko ya kijenetiki, yanayotokea kwa nadra sana kwa mwanadamu.

Hiyo manaa yake ni kwamba mtu huyo daima hana hisia za maumivu kabisa, hana shaka wala kupata hofu anapoungua mwilini au chochote kinachomuumiza ngozi.

Hali ilikuwa hivyo mpaka alipotimiza miaka 65, ndipo alipogundua kuwa yuko tofauti, pale madaktari waliposhindwa kuamini kuwa hahitaji dawa za kuondoa maumivu, baada ya kufanyiwa upasuaji mkubwa. Ni upasuaji uliofanyika mkononi mwake, madaktari walimtahadharisha kwamba ategemee kupata maumivu baada ya upasuaji, lakini kazi hiyo ilipokamilika, mama huyo hakuhisi maumivu ya aina yoyote.

Ni jambo lililomstua na kumshangaza daktari wake wa dawa za usingizi, Devjit Srivastava, aliyelazimika kumpeleka kwa wataalamu wa masuala ya maumbile na jenetiki, katika vyuo vya London na Oxford, Uingereza kwa uchunguzi zaidi kulikoni, hali ni hivyo?

Baada ya vipimo, walibaini kuwa ana mabadiliko kwenye vinasaba vyake, vinavyomfanya asihisi maumivu kama ilivyo kwa watu wengi.

### HALI INAYOSHANGAZA

Mama huyo anasimulia mkasa wake namna madaktari hawakuamini kwamba hahitaji dawa ya kuondoa maumivu baada ya upasuaji.

"Tulizungumza kabla ya kwenda kwenye chumba cha upasuaji na nikawahakikishia kuwa, sitahitaji dawa za kuondoa maumivu," anasema mama huyo na kuongeza:

"Alipogundua kuwa sikuwahi kumeza dawa za maumivu, alitazama historia yangu ya kitabibu na kugundua kuwa sikuwahi kutumia dawa za kuondoa maumivu."

Mwanamke huyo, Jo, anaeleza mkasa huo ulimfikisha hatua ya kuamini kwamba, hakuwa sawa kiafya kinyume na analivyoamini awali.

"Nikikumbuka huko nyuma, nikagundua sikuwahi kuhitaji dawa za kuondoa maumivu. Lakini kama huzihitaji, huwezi kuhoji kwa nini huzihitaji," anasimulia na kuingeza:

"Wewe ni wewe ulivyo, mpaka pale mtu mwingine atakapobaini vinginevyo. Nilikuwa mwenye furaha, ambaye sikubaini kama kuna tofauti yoyote mwilini mwangu."

Pia, anasema hakuhisi maumivu yoyote hata wakati anajifungua, akikumbuka kwa kauli: 'Halikuwa jambo la kawaida, lakini sikuwa na maumivu, kwa kweli niliifurahia hali hii."



Jo Cameron (kulia), akiwa na mama yake na mumewe. **PICHA: MTANDAO.**

> **Alikuwa akitetemeka kweli kweli, lakini aliweza kutulia baadae. Mimi hali hii hainitokei...**

### UPONAJI WAKE

Madaktari wanaamini kuwa Jo atakuwa na uwezo wa kupona haraka sana kuliko kawaida. Jeni zake zinamfanya asahau na asiwe mwenye hofu

"Inaitwa jeni zenye kuleta furaha au zinazosahau. Nimekuwa nikiwaudhi wengine kwa kuwa na furaha na mwenye kusahau maisha yangu yote. Nina sababu sasa," anaeleza.

Jo anasema, hivi karibuni alikuwa na uvimbe mdogo baada ya kujigonga akiwa kwenye gari, lakini hali hiyo ambayo wengi wangeiona mbaya sana, haimkumshtua hata kidogo.

"Sina 'adrenalini' (aina Fulani ya homoni ya kibinadamu).Lazima uwe nayo, ili uweze kukupa tahadhari kuhusu hali uliyo nayo. Ni sehemu ya hali ya kuwa binadamu, lakini siwezi kubadili hali hii."

Dereva mwingine, anasema: "Alikuwa akitetemeka kweli kweli, lakini aliweza kutulia baadae. Mimi hali hii hainitokei...sikuwa mimi ni mwerevu, ni kwamba hali ya hofu haijitokezi."

Watafiti wanasema, inawezekana duniani kuna watu wengine wa aina ya Jo, mtaalamu Dokta Srivastava, akilifafanya hilo kwa kauli: "Mmoja kati ya wagonjwa wawili baada ya upasuaji, hupata maumivu kidogo au maumivu makali, pamoja na kuwapo kwa uboreshwaji wa dawa za kuondoa maumivu."

Anasema, alichokifuatilia kwa Jo, yamo kwenye maandiko ya utafiti wa British Journal of Anaesthesia, ulioandikwa na Dk. Srivastava na Dokta James Cox.

***• Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za Mtandao.***

# Aliyezirai miaka 27 azinduka anajiweza

MWANAMKE kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu(UAE), aliyeumia sana katika ajali ya gari iliyotokea mwaka 1991 na kupoteza fahamu, amestaajabisha wengi baada ya kuamka akiwa amepona, kutoka kwenye 'koma' iliyomchukua miaka 27.

Munira Abdulla, alipata ajali akiwa na umri wa miaka 32 na kupata jeraha katika ubongo, baada ya kugongwa na basi wakati alipokuwa anaelekea kumchukua mtoto shuleni.

Mwanawe, Omar Webair, alikuwa na miaka minne wakati waalipopata ajali. Omar alikuwa aliyekuwa ameketi katika kiti cha nyuma, hakujeruhiwa hata kidogo na alikutwa akiwa amekumbatiwa na mama yake.

Munira alijeruhiwa vibaya, lakini mwaka jana akiwa katika hospital nchini Ujerumani, alianza kurejesha fahamu taratibu.

Hivi sasa Omar, akiwa mtu mzima ameweka wazi kuhusu ajali walioipata na kuelezea utaratibu wa matibabu ya mama yake yalivyochukua miaka mingi.

### ALINIKUMBATIA NISIUMIE

"Sikuwahi kukata tamaa, kwa sababu kila siku nilihisi kuwa kuna siku mama yangu ataweza kuamka," anaeleza Omar na kuongeza sababu inayomfanya asimulie mkasa wao, ni kuufahamisha umma kuacha kukata tamaa, kwa wagonjwa wanaofika hatua ya mama yake, haimaanishi kufa.

Mama mkwe wa Munira, ndiye aliyekuwa dereva na kijana huyo anaendeleza simulizi: " Mama yangu alikuwa amekaa na mimi katika kiti cha nyuma.Alipoona tunakaribia kupata ajali, alinikumbatia,ili kuniokoa katika ajali hiyo."

Katika ajali hiyo, Omar hakuumia bali alibaki na jeraha dogo kichwani na anaongeza kuwa mama yake alichelewa kupata matibabu kwa saa kadhaa.

### MIAKA YA MATIBABU

Munira alifikishwa hospitali baada ya saa, baadae alihamishiwa mjini London, Uingereza akiwa amepoteza fahamu, lakini alikuwa na uwezo wa kuhisi maumivu.

Baada ya muda, alirudishwa mjini Al Ain UAE, alikoishi na mtoto wake Omar na kuendelea kuzunguka katika vituo mbalimbali vya afya kulingana na bima ya afya aliyokuwa nayo.

Alikula kwa kutumia mirija, huku akifanyiwa mazoezi na vipimo vya viungo, kuhakikisha misuli yake haidhoofiki, kwa kuwa hatembei.

Mwaka 2017, familia ilipokea msaada kutoka serikalini, kumuwezesha Munira kwenda kutibiwa Ujerumani alikofanyiwa upasuaji mara kadhaa, kurekebisha mkono uliopunguzwa na akawekewa sawa misuli ya mguu.

### AZINDUKA WODINI

Baada ya mwaka mmoja, siku moja mtoto wake alikuwa anazozana ndani ya chumba alichokuwamo mama yake hospitalini, ghafla mama aliamka.

"Kulikuwapo kutoelewana katika chumba alichokuwa amelazwa na alihisi kuwa niko hatarini, jambo lililomfanya ashtuke," Omar anasimulia, akisema:

"Alikuwa anahangaika kutoa sauti na nilikuwa nahangaika kuita madaktari, ili wampime na walisema kuwa kila kitu kilikuwa sawa".

"Siku tatu baadaye, niliamka nikasikia mtu ananiita kwa jina langu. Alikuwa yeye, alikuwa anaita jina langu. Nilikuwa kama ninapaa kwa furaha.

'Kwa miaka mingi nimekuwa nikiota siku hii ifike na jina langu lilikuwa neno la kwanza kulitamka baada ya miaka 27," Omar alieleza.

Huo ukawa mwanzo ambao baadaye akawasiliana na sasa baada ya maumivu ya muda anaweza kuzungumza.

Mama huyo amerudi nyumbani kwake Abu Dhabi, UAE anakoendelea kutibiwa viungo kwa mazoezi na ushauri, hasa namna ya kukaa na kufanya kazi misuli iwe imara.

Kitaalamu, inaelezwa watu wanaopata ufahamu baada ya 'koma' ya muda mrefu, mara nyingi tatizo lao huwa linatokana na madhara katika ubongo. **BBC**



## Sokoni waiomba TRA makadirio

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Mwanjelwa jijini Mbeya wameiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani hapa kutoa makadirio madogo ya kodi ambayo yanaendana na biashara zao.

Wamesema kutakiwa kulipa kodi kubwa kutawafanya washindwe kumudu kulipa.

Wito huo ulitolewa juzi na wafanyabiashara hao, wakati mkutano na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya, Afrey Nsomba, na kumweleza kuwa wanafanya biashara zao kwenye mazingira magumu.

Abigael Asumwisye, alisema kwa sasa kuna makadirio makubwa ya kodi ukilinganisha na kipindi cha nyuma, hali inayopelekea wafanyabiashara kuhoji mabadiliko hayo bila kupatiwa majibu ya kuridhisha kutoka mamlaka hiyo.

Alisema makadirio ya kodi inayotolewa na TRA hayaendani na uhalisia wa biashara zao na kuiomba Mamlaka kuangalia upya makadirio ya kodi inazotoza.

"Tunaiomba Mamlaka ya Mapato kuangalia upya makadirio ya kodi inazotoza... hii itasaidia kujenga mahusiano mazuri kati yetu na kufanikisha malengo ya serikali ya ukusanyaji kodi kikamilifu kwa kutoa elimu kwa wafanyabiashara," alisema Mwakanyamale.

Aidha, wafanyabiashara hao wamelalamikia kauli mbaya zinazotolewa na baadhi ya watumishi wa TRA, ambazo wanasema zinasababisha wafanyabiashara kushindwa kuhoji na kupata majibu kwenye masuala mbalimbali ya biashara na kodi.

# Wawekezaji mbegu za mazao waishauri serikali

**Na Grace Mwakalinga,**
SONGWE

WAWEKEZAJI wa mashamba ya kilimo cha mbegu za mazao mkoani Songwe, wameishauri Serikali kupunguza kiwango cha uingizaji wa bidhaa hiyo mpya kutoka nje ya nchi.

Badala yake wameshauri ijikite kutangaza mbegu zinazozalishwa na wawekezaji wa ndani kwa kuzingatia utafiti uliofanywa na wataalamu wa Wizara ya Kilimo.

Hayo yalisemwa na Mwekezaji Uzalishaji Mbegu Mpya, Mary Mgonja, wakati wa ziara ya kutathmini hali ya uzazi wa mbegu za mazao za mahindi, mtama, alizeti na mikunde katika mashamba ya Namburi Kata ya Magamba wilayani Mbozi.

Mary alisema bado kiwango cha uagizaji mbegu mpya toka nje ni kikubwa hali inayowakatisha tamaa wawekezaji wa ndani kuendelea kunufaika na matokeo mazuri ya utafiti mbalimbali unaofanywa na wataalam kutoka wizarani.

"Mbegu zinazoingizwa nchini huuzwa kwa bei ghali ukilinganisha na gharama za mbegu zinazozalishwa na kampuni za ndani, wakulima wengi hushindwa kumudu gharama, wakati mwafaka kwa serikali kutoa kipaumbele kwa wazawa kuuza pembejeo zao ambazo zitamnufaisha kila mkulima na kuzipata kwa wakati," alisema Mary.

Mkuu wa Wilaya Mbozi, John Palingo, alikiri uingizwaji wa mbegu za kilimo kutoka nje ya nchi ukilinganishwa na mbegu zinazozalishwa na wazawa nchini, na kusema ni wakati mwafaka kwa serikali kutoa kipaumbele matumizi ya mbegu zinazozalishwa nchini.

Alisema Wilaya ya Mbozi inawakaribisha wataalamu na watafiti wa kuzalisha mbegu kufungua viwanda ambavyo vitakuwa msaada kwa wakulima.

Naye Mkurugenzi wa Sera, na Sheria za kusimamia mwenendo wa upatikanaji wa mbegu bora kutoka Wizara ya Kilimo, alisema kwa sasa hakuna haja ya kuagiza Mbegu kutoka nje, badala yake Tanzania ina uwezo wa kupeleka mbegu nje ya nchi.

Alisema Serikali inakabiliwa na changamoto ya mashamba ya kilimo cha vizazi mbegu nchini isipokuwa nyanda za juu kusini, hivyo uzalishaji wa mbegu nchini utakuwa mwarobaini na kwamba mbegu hizo zitakidhi mahitaji ya wakulima.



Wachimbaji wadogo wa madini katika Mji wa Mkwajuni, wilayani Songwe, wakisikiliza kwa makini mafunzo ya elimu ya afya na usalama kwenye migodi, yaliyotolewa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), wilayani humo, mkoani Songwe jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Vitambulisho vya taifa kamili kwa asilimia 80

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) mkoani Mbeya imesema zoezi la utoaji vitambulisho limefanikiwa kwa asilimia 80 na kuhimiza watumiaji wote wa simu za mkononi nchini kujisajili upya kwa kutumia alama za vidole kama agizo jipya linavyotaka.


Hayo yalisemwa jana na Msajili wa NIDA mkoani Mbeya, Alavuya Ntalima, alipokuwa akizungumza na Nipashe juu ya zoezi la utoaji wa vitambulisho hadi sasa ambapo alisema zoezi hilo limefanikiwa kwa asilimia 80. Alavuya alisema licha ya zoezi hilo kufanikiwa kwa asilimia 80, lakini bado kuna changamoto ikiwamo uchelewaji wa baadhi ya vitambulisho vya wananchi ambao walijiandikisha tangu mwaka jana.

Licha ya kuchelewa kwa vitambulisho hivyo, lakini alisema kuna utaratibu mpya umetolewa wa namna ya kupata vitambulisho hivyo, alisema huduma hiyo inapatikana kwenye simu za mikononi.

"Huduma hii inahitaji kusajili upya laini za simu na wananchi watakiwa kuwa na Sh. 100 ili kupata namba ya kitambulisho na kuepusha usumbufu wa kufika katika ofisi za NIDA," alisema Avuya.

Aliwahimiza wananchi kutumia mfumo huo ambao ni rahisi na utawawezesha kupata vitambulisho kwa haraka ukilinganisha na mfumo uliokuwapo awali.

Aidha, alisema wananchi waliojisajili kwa ajili ya kupata vitambulisho vyao tangu mwaka jana wafike kwenye ofisi za kata ili kuchukua vitambulisho. Wananchi mkoani Mbeya wameilalamikia NIDA kuchelewesha utoaji wa vitambulisho na wanachi wengi mpaka sasa hawajapata. Miongoni mwao, Fredy Lucas, alisema NIDA mpaka sasa haijatoa vitambulisho maeneo mengi, na mfumo huo mpya hauwezi kufanikiwa kwa sababu hakuna elimu iliyotolewa na mfumo wake ni mgumu.





## 200 wafunzwa matumizi kemikali za viwandani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAJASIRIAMALI zaidi ya 200 wamejitokeza kupata mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya matumizi sahihi ya kemikali za viwandani.

Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) Mkoa wa Dodoma, Sempeho Manongi, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa waliopatiwa mafunzo hayo ni miongoni mwa wanaotengeneza bidhaa mbalimbali zikiwamo sabuni na batiki.

"Kuna wazalishaji wa bidhaa za sabuni, vipodozi, batiki na hata vyakula ambao kila siku wanatumia kemikali, tuliona ni vyema wajue matumizi sahihi ya kemikali hizo ili kujiepusha na madhara, usalama wao, uhifadhi wake kwenye maeneo ambayo ni sahihi, kutumia kemikali zinazokubalika kwa ajili ya kulinda afya za watumiaji na walaji," alisema.

Manongi alisema mafunzo hayo yalitolewa na Sido Mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu Kanda ya Kati, Shirika la Viwango (TBS) na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

Alisema wanatarajia kuona wajasiriamali wanafanya shughuli zao kwa kufuata kanuni ili kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa lengo la kuwalinda watumiaji wa bidhaa hizo.

Alisema malengo mengine ya mafunzo hayo ni kuwaimarisha katika utunzaji na ubebaji wa kemikali husika wakati wanapoendelea na uzalishaji wa bidhaa, kuongeza ubora na ufanisi katika uzalishaji.

"Malengo mengine ni kuongeza ushindani wa wajasiriamali katika kufikia masoko mbalimbali ndani na nje ya nchi, kuimarisha uwezo wa wasambazaji na watumiaji wa kemikali viwandani katika kuhakikisha matumizi endelevu yenye tija katika mnyororo wa uzalishaji na kuwajengea uwezo wazalishaji katika matumizi salama na bora na ya uhakika ya kemikali," alisema.

Manongi alisema matumizi salama na bora ya kemikali yanaendana na mwelekeo wa serikali ya awamu ya tano ya ujenzi wa Tanzania ya Viwanda katika kufikia uchumi wa kati.

Alisema Dodoma ikiwa ni makao makuu ya nchi, ni kitovu cha utekelezaji wa dhana hiyo kwa vitendo kwa matumizi sahihi ya kemikali za aina mbalimbali viwandani.

"Hii itawahakikishia wazalishaji na walaji, usalama wa kiafya na kuongeza wigo wa soko wa bidhaa wanazozalisha baada ya kukidhi vigezo vya ubora," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Biashara wa Sido Mkoa wa Dodoma, Crispin Kapinga, alisema zaidi ya asilimia 80 ya washiriki wa mafunzo hayo walikuwa wanawake.

Alisema wajasiriamali wanatakiwa kujua matumizi sahihi ya kemikali hizo na kuwataka wanaotengeneza bidhaa zinazotumia kemikali, kuhakikisha wanapata mafunzo kwenye taasisi na si kujifunzia mitaani ili kuepuka bidhaa hafifu kuingia sokoni.

# Askofu ashauri wapinzani kurejea CCM

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Kimethodost Tanzania, Joseph Bundala, amewashauri wanachama wa vyama vya upinzani nchini, kurejea Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokana na kile alichodai kutokuwa na uhuru wa kufanya siasa katika vyama wanavyovitumikia kwa sasa.

Kiongozi huyo wa kiroho alitoa rai hiyo alipozungumza na waandishi wa habari juu ya mwenendo wa hali ya kisiasa nchini.

Askofu Bundala alisema kwa sasa hali ya kisiasa imebadilika na wapinzani hawana uhuru wa kufanya kazi zao za kisiasa, hivyo ni bora wakarudi CCM ili kujenga nchi kwa pamoja na kwa umoja.

Pamoja na kuwapo kwa changamoto hiyo, askofu huyo alisema serikali ya awamu ya tano imefanya mambo mengi ambayo yalikuwa yakilalamikiwa na wapinzani.

"Pamoja na mambo mengine, yapo mambo mengi ambayo wapinzani walikuwa wakiyapigia kelele, lakini serikali hii imefanikiwa kuyafanyia kazi na sasa tunaona mafanikio mengi," alisema.

Aliwataka Watanzania kuendelea kumwombea Rais John Magufuli kutokana na utendaji wake ambao kwa sasa umekuwa ukiwagusa karibu watu wote bila kujali itikadi zao za vyama.

Alisema Rais pamoja na watendaji wake wanatakiwa kuombewa ili wafanye kazi zao kwa ufanisi na kwa maadili ya kiroho ambayo yataongeza maendeleo ya taifa.

Askofu huyo pia alishauri wakulima waliobahatika kupata mazao mwaka huu, wahifadhi chakula kwa kuwa maeneo mengi nchini yamekumbwa na ukame.

Kiongozi huyo wa kanisa pia alisema kuna haja kuiombea nchi ifanikishe uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika.




Mbunge wa Jimbo la Dodoma, Athony Mavunde (wa tatu kushoto), akimkabidhi Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof Davids Mwamfupe (wa pili kushoto), vifaa na vifaranga vya kuku vyenye thamani ya Sh. milioni 68, kwa ajili ya vikundi 37 vya jimbo hilo, kupitia mfuko wa jimbo, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mpango Elimu Jumuishi wasaidia wenye ulemavu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MPANGO wa Elimu Jumuishi nchini, umewawezesha watoto wenye ulemavu kupata fursa ya elimu jirani na maeneo wanayoishi.

Meneja wa Shirika Lisilo la Kiserikali la International Aid Services (IAS), Allan Kamnde, aliyasema hayo katika semina ya wadau wa maendeleo Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

Kamnde alisema mpango huo umesaidia watoto wenye ulemavu kupata fursa ya elimu jirani na maeneo wanayoishi tofauti na walivyokuwa awali walipokuwa wamejitenga kwa kuwa na shule zao binafsi.

"Elimu Jumuishi ni utaratibu wa upatikanaji wa elimu kwa watoto wote bila kujali hali ya ulemavu, kiuchumi, kidini, rangi au kabila na jinsia, wote wanapata elimu bila kubaguliwa," alifafanua. Alisema shirika lao kwa kushirikiana na serikali wamekuwa wakiendesha shughuli mbalimbali kwa lengo la kupunguza vikwazo katika upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu nchini.

Alibainisha kuwa kupitia mafunzo wanayofanya, wanawashirikisha walimu, wazazi wa watoto wenye ulemavu na viongozi wa serikali na kisiasa katika maeneo ambayo shirika hilo linatekeleza mradi wake, kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili watoto hao.

Alizitaja kazi zingine wanazofanya pamoja na serikali kuwa ni utambuzi wa watoto wenye ulemavu na kutoa mafunzo kwa walimu kwenye maeneo ya mradi wanapofanya kazi.

Jukumu lingine ni ukarabati wa miundombinu ya shule, uchangiaji wa thamani za shule kama magodoro, mashuka na upimaji wa watoto wenye ulemavu. Alisema jukumu lingine la shirika lao ni uhamasishaji na utetezi wa haki za watoto kupitia mabaraza ya watoto.

Alibainisha kuwa jukumu lingine ni kufanya ufuatiliaji wa ushiriki wa wananchi katika upatikanaji wa elimu kwa watoto wote bila ubaguzi. Alisema shirika hilo linafanya kazi katika mikoa ya Singida, Katavi, Rukwa na Dodoma. Mwalimu Nasibu Khatibu wa Shule ya Msingi Buigiri wilayani Chamwino, alisema shule yao ina watoto mchanganyiko, lakini miundombinu imekuwa kikwazo kwa wenye ulemavu.





Msajili mstaafu wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Boniface Muhegi (kushoto), akimkabidhi cheti Mkurugenzi Mtendaji wa Gemini Engineering & Construction, Enock Koola, baada ya kuwa mwanachama mpya wa Chama cha Makandarasi Wazalendo Tanzania (ACCT), wakati wa Mkutano Mkuu wa Nane wa chama hicho, uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shein akumbusha wajibu vyuo vikuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Suza) kina dhima kubwa ya kutoa taaluma bora inayoambatana na kufanya utafiti kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizoko katika jamii.

Akizungumza katika mahafali ya 14 ya chuo hicho, Dk. Shein alisema kufanya utafiti ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya vyuo vikuu ili kutoa mchango wa chuo kitaaluma na kupandisha hadhi ya ubora wa chuo chenyewe.

Alikitaka chuo hicho kiendelee kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech), iliyo na wajibu wa kuwawezesha watafiti mbalimbali nchini kufanya utafiti wanaokusudia.

Dk. Shein alisema chuo kikuu hicho kinao wajibu wa kutafuta fedha za kufanya utafiti kutoka vyanzo mbalimbali kwa kuwa utafiti ni miongoni mwa majukumu ya chuo hicho, akieleza kuwa hakuna maendeleo bila ya utafiti.

Alisema utafiti ni ngazi muhimu kwa wanachuo wa mafunzo ya uzamili na uzamivu ambao huwasaidia kuhitimu masomo yao, hivyo kukihimiza chuo hicho kujiandaa kuchapisha majarida ya kitaaluma ambayo wahadhiri na wanachuo wa ngazi ya uzamili na uzamivu watapata fursa ya kutuma makala zao zinazotokana na utafiti waliofanya. Aliutaka uongozi wa chuo hicho kuwaweka sawa baadhi ya wahadhiri wachache ambao hawatekelezi majukumu yao ipasavyo pamoja na wafanyakazi wote wanaojaribu kufanya kazi zao kinyume cha utaratibu.

Alisema wahadhiri na wafanyakazi wa namna hiyo hawatimizi wajibu wao vizuri na hawachangii maendeleo ya chuo na hawana uzalendo.

Alisema kuwa ili mafanikio yapatikane, ni vyema kukadumishwa umoja na mshikamano baina ya wahadhiri, wafanyakazi, wanafunzi na washirika wote wa chuo hicho huku akiwataka kujiepusha na mambo yanayoweza kuleta mifarakano.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof Idissa Rai, alisema mahafali ya mwaka huu yameandika historia mpya kwa chuo hicho kutokana na kutoa wahitimu wa fani ya udaktari.

Alisema uanzishaji wa masomo hayo ni utekelezaji wa agizo la Rais alilolitoa katika mahafali ya mwaka 2011, kwa lengo la kuhakikisha Zanzibar inajitegemea kwa wataalamu wa fani hiyo.

Alisema hatua ya chuo hicho kutoa wahitimu 25 wa fani hiyo inatoa mwelekeo mzuri wa kufikia malengo hayo.

Alisema kwa sasa chuo kinajipanga kuanzisha fani ya udaktari wa meno, sambamba na malengo ya baadaye ya kuanzisha masomo ya ubaharia.

Katika mahafali hayo, jumla ya fani za masomo 56, zilitoa wahitimu 1,940 (asilimia 58 ya wahitimu ni wanawake) na kwa mara nyingine mwanafunzi bora alikuwa mwanamke.

# 'Hakuna virusi pori vya polio Zanzibar'

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR ni miongoni mwa nchi zisizo na virusi pori vya polio vinavyosababisha ulemavu kwa watoto wadogo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya wiki ya chanjo, Naibu Waziri wa Afya, Harous Said Suleiman, alisema mafanikio hayo yametokana na kufanikiwa kwa chanjo watoto walio chini ya umri wa miaka miwili.

Alisema pamoja na mafanikio hayo, bado zipo changamoto za watoto wachache ambao hawajapata chanjo kabisa au hawajakamilisha ratiba zao za chanjo.

Alisema watoto hao wako katika hatari ya kupata maambukizio ya magonjwa na kuhatarisha jamii.

Alisema ni muhimu kuhakikisha kila mtoto anapata chanjo zake zote kwa wakati ili kumlinda dhidi ya maambukizo ya magonjwa mbalimbali.

Alisema imethibitika chanjo ni tiba mwafaka na ya gharama nafuu katika kutokomeza maradhi na kupunguza vifo vya watoto.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano katika kukamilisha utoaji wa chanjo ambao ulianza jana hadi Aprili 30, mwaka huu kwa watoto chini ya miaka miwili na wasichana wenye miaka 14, huduma zikitolewa katika vituo vyote vya afya vya serikali.

# Viongozi CCM wabanwa kwa kumiliki mali za chama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Magharibi Unguja, Mohamed Rajabu Soud, amewataka wabunge, wawakilishi na madiwani wa mkoa huo kuhakikisha mali zote walizonunua kwa ajili ya shughuli za majimbo, hati zake ziandikwe umiliki wa CCM na siyo majina yao.

Akizungumza na kamati ya siasa ya mkoa huo na kukagua utekelezaji wa ilani ya chama hicho katika Jimbo la Bububu, Soud alisema hatowavumilia baadhi ya viongozi wanaonunua vifaa mbalimbali kwa ajili ya majimbo na kuzimiliki kwa majina yao badala ya jina chama.

Alisema chombo pekee kinachomiliki mali zote za chama ni Baraza la Wadhamini wa CCM na ni lazima mali zote ziwe chini ya taasisi hiyo.

"Nawaagiza wabunge, wawakilishi na madiwani wote katika mkoa wangu, mali zote walizonunua kwa ajili ya CCM, basi ziwe na jina la taasisi hii na sitopenda kuona gari limenunuliwa kwa ajili ya jimbo wakati kadi ya umiliki inasomeka jina la aliyeinunua badala ya CCM," alionya.

Kiongozi huyo pia aliwataka viongozi na wanachama wa chama hicho kuvunja makundi yasiyokuwa rasmi kwa mujibu wa miongozo na kanuni za kikatiba.

Alisema kuna baadhi ya majimbo bado kuna makundi ya kufitinisha, hali inayokwamisha harakati za maendeleo kwa kuwa baadhi ya huduma za msingi haziwafikii wananchi kwa wakati kutokana na athari za makundi hayo.

Alisema uchaguzi unapomalizika ndani ya chama, makundi yote yanapaswa kuvunjwa na kubaki kundi moja la CCM linalotoa nafasi pana kwa viongozi wanaochaguliwa kuwatumikia wananchi kwa uadilifu.

Aliwataka viongozi wa Jimbo la Bububu kuendelea kufanya kazi kwa kasi zaidi na kutatua changamoto za wananchi ili CCM ishinde kwa kura nyingi katika uchaguzi mkuu ujao.

Kiongozi huyo pia alieleza kuridhishwa kwake na utendaji wa viongozi hao na kuwataka wazidishe kasi ya kutekeleza ilani ya CCM hasa katika miradi mbalimbali ya kijamii ambayo bado haijatekelezwa ipasavyo.

Mbunge wa jimbo hilo, Mwantakaje Haji, aliwataka wananchi kuitunza na kuithamini miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa ndani ya jimbo ili iwanufaishe wananchi wote.

Aliahidi kuyafanyia kazi kwa wakati maelekezo aliyopewa na Kamati ya Siasa ya CCM ya mkoa huo ili kuendelea kutekeleza ilani ya chama hicho kwa ufanisi zaidi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 24/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATATU tarehe **29/04/2019** kampuni ya WULKAN ENG itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka ARUSHA kuelekea NAMANGA gari hilo lenye namba za usajili: **T827BCN,T741 CPB,T985 ABJ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 17
   Upana –mita 3
   Kimo – mita 3.2
3. Njia itakayotumika **ARUSHA** hadi NAMANGA kupitia NGARAMTONI gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**


Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

215193302

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI
IDARA YA UHAMIAJI

**MAOMBI YA URAIA**



**BW. AMAN PREET SHARMA** anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.Ni raia wa India na nchi atokayo ni India.

Yeyote mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa Afisa Uhamiaji Mkoa wa Dodoma, S.L.P 558.

115193402

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ZAHOR MOHAMED ISSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya CANTER yenye namba za usajili T289CLU. Chassis namba FE315BD442616. Engine NO.4D35302045.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/301/2019.**

115194302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - MWANZA**
**SHAURI NA. 410 LA 2018**
**MAGRETH L. IFUNYA........................MDAI**
**DHIDI YA**

**1. JUMA KIANGO**
**2. JACKSON BAHATI**
**3. GRACE MURUNGU ..........................................WADAIWA**
**4. JOSEPH SENDE**
**5. ELDANG AUCTIONEER & GENERAL BROKER**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

KWA: JUMA KIANGO
JACKSON BAHATI
GRACE MURUNGU

**ELDANG AUCTIONEER & GENERAL BROKER**

Mnafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yenu katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza. Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 27/05/2019 katika Chumba cha Baraza, barabara ya Posta. Jengo liko mkabala na Mahakama Kuu ya Biashara, Tanzania.

Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, Wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.

**KAENI-** Mkijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 17/04/2019.

115194102

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo: HAI KATI**

**Usimamizi wa Mirathi 09/2019**

Ombi la JANETH EMANUELY MBOWE Kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu EMANUELY WILLIAM MBOWE
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa

Kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo ….23…/04/….19………kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe ….10….04….19…………………

115194202

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya MAKOLE**
**Usimamizi wa mirathi NA. 26/2019**
**Ombi la MARY LEONARD LYIMO**

Msimamiliz wa mirathi ya marehemu LESSION ISRAEL RAYASE

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 3/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyoupo mahakamni waweza kukaguliwa

Tarehe 18/04/2019

115193802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;98/2019**

Ombi la MSIMBE NG'ATIGWA MEZA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NG'ATIGWA MEZA KHALFAN

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/05/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/03/2019.

215193102

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**Mehreen Mohamedaslam** Barde anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba T998 DNB aina ya TOYOTA PASSO,

yenye chasis namba ONC100021978, engine namba KJ1296619.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa:**
**KJN/B.I/I/VOLXI/6488/2019**

115192702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**


Usimamizi wa mirathi No; 75/2019
Ombi la **BLANCA THADHEI URASA NA SUZANA ORESTUS MWONJA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ORESTUS PIUS MWONJAWatu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 14/03/2019.

215192402

---

**KUPOTEA KWA PASSPORT/HATI YA KUSAFIRIA**



Rashid Seif Azan anatangaza kupotea kwa Passport yake yenye namba **AB790125** iliyotolewa na Ofisi za Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2016.

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**KW/K/B.I/I/VOL.265**

115192802

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**Walpha Tours & Safari's Ltd** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba T974 BTS aina ya TOYOTA MARK II, yenye chasis namba EX1106082611, engine namba IGFE876.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KJN/B.I/I/VOLXI/6488/2019**

115192602

TANGAZA NA NIPASHE

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

TANGAZO

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.03.2019 (Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA 31.03.2019 | ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.12.2018 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 5,657 | 3,744 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,055 | 17,681 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 28,396 | 23,368 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 27,692 | 27,511 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | - | 11 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 98,585 | 98,573 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,903 | 1,412 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,242 | 1,279 |
| # | **Jumla ya Mali** | **177,530** | **173,579** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,272 | 1,272 |
| 18 | Amana za Wateja | 134,886 | 132,158 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 89 | 137 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 73 | 41 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 20 | 20 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,126 | 896 |
| 28 | Madeni | - | - |
| # | **JUMLA YA DHIMA** | **137,466** | **134,524** |
| # | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **40,064** | **39,055** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 941 | 937 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 24,203 | 21,987 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,009 | 2,147 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,911 | 3,984 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **40,064** | **39,055** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 6,527 | 7,209 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,567 | 6,567 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,362 | 2,151 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 23% | 23% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7% | 7% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 74% | 76% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 56% | 57% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 87% | 86% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 2% | 3% |
| (vii | Ongezeko la Mali | 2% | 2% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2019

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO YA MWAKA SASA 31.03.2019 | ROBO YA MWAKA LINGANISHI 33.03.2018 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.03.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.03.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,498 | 3,376 | 3,498 | 3,376 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,109 | 1,235 | 1,109 | 1,235 |
| **3** | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,389** | **2,141** | **2,389** | **2,141** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 210 | 459 | 210 | 459 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **370** | **478** | **370** | **478** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 167 | 157 | 167 | 157 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 201 | 320 | 201 | 320 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 1 | 2 | 1 | 2 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba:** | **1,174** | **1,292** | **1,174** | **1,292** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 578 | 359 | 578 | 359 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 16 | 53 | 16 | 53 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 579 | 880 | 579 | 880 |
| | 7.4 Other Provision | - | - | - | - |
| **8** | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,375** | **868** | **1,375** | **868** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 366 | 363 | 366 | 363 |
| **10** | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,009** | **505** | **1,009** | **505** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,009** | **505** | **1,009** | **505** |
| **13** | Idadi ya Waajiriwa | **50** | **48** | **50** | **48** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 101 | 50 | 101 | 50 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 4 | **4** | **4** | **4** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.26% | 0.29% | 2.26% | 0.29% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 10.15% | 1.31% | 10.15% | 1.31% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 42.53% | 47.17% | 42.53% | 47.17% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6.33% | 1.48% | 6.33% | 1.48% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31.03.2019 (Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | | ROBO YA MWAKA YA SASA | ROBO YA MWAKA ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **31.03.2019** | **31.12.2018** | **31.03.2019** | **31.03.2018** |
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1,375 | 388 | 1,375 | 868 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | | | | |
| | -Hasara katika Mali | 260 | 660 | 260 | 520 |
| | -Prior Period Adjustment | - | 50 | - | (116) |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (222) | (10,805) | (222) | (745) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,728 | 3,325 | 2,728 | 1,571 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 215 | 908 | 215 | (3,938) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 4,901 | 14,030 | 4,901 | (3,379) |
| | -Kodi Iliyolipwa | (366) | (263) | (366) | (363) |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | (912) | 17 | (912) | (445) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **7,980** | **8,311** | **7,980** | **(6,027)** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | (13) | (1) | (13) | (5) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | (5,029) | (11,380) | (5,029) | 668 |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (ainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(5,041)** | **(11,382)** | **(5,041)** | **663** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV** | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **2,938** | **(3,071)** | **2,938** | **(5,363)** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 31,307 | 34,378 | 31,307 | 37,328 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **34,245** | **31,307** | **34,245** | **31,964** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.03.2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengine ya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,009 | - | - | - | 1,009 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 73 | (73) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (3) | - | 3 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **25,213** | **3,911** | **940** | **-** | **40,064** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | 10,000 | - | 22,271 | 4,068 | 781 | - | 37,120 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,147 | - | - | - | 2,147 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 84 | (84) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (156) | - | 156 | - | - |
| Mengineyo | - | - | (212) | - | - | - | (212) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2019**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir (Mkurugenzi Mtendaji) | | 15th April, 2019 |
| Deogratias Edward Ndushi Mkuu wa Fedha | | 15th April, 2019 |
| Mwita Mohamed Mwita (Mkaguzi wa Ndani) | | 15th April, 2019 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni | | 15th April, 2019 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava | | 15th April, 2019 |

215194602




# JOVIC KUTUA REAL

**MUNICH,** Ujerumani

MKURUGENZI wa Michezo wa Eintracht Frankfurt, Fredi Bobic anaamini kwamba kuna uwezekano mkubwa wa nyota wake, Luka Jovic kujiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaj huyo wa kimataifa wa Serbia amejipambanua kama mmoja wa nyota wanaotamba Ulaya kwa sasa, huku akiwa amefunga mabao 25 kwenye michuano yote msimu huu, na pia kukiwa na ofa kutoka Bayern Munich, Liverpool, Barcelona na Real Madrid.

Na wakati majaliwa ya Jovic yakiwa hayaeleweki kipindi hiki cha majira ya joto, Bobic amebainisha kwamba ni kitu kisichowezekana kumbakisha mchezaji huyo kutokwenda Real Madrid.

"Kuna uwezekano kwamba, Jovic atasajiliwa Real Madrid," amesema Bobic, akinukuliwa na Marca.

"Natumaini atabaki Eintracht, lakini ukweli ni kwamba kama Real Madrid wanataka kumsajili wanaweza kufanya hivyo bila tatizo lolote."

Wakati Los Blancos pia watapata ushindani kutoka Liverpool na Barcelona, ambapo Jovic amekuwa akiwaniwa na klabu hizo.

Goal.com imebainisha kwamba Bayern Munich inajiandaa kuingia kwenye mbio za kuwasajili mwishoni mwa msimu huu.

## Hudson-Odoi avutia pumzi kusepa Chelsea

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI kinda wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi amekataa kufanya maamuzi kuhusu majaliwa yake ya baadaye klabuni hapo baada ya kuumia kifundo cha mguu kwenye mchezo dhidi ya Burnley.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi sita kutokana na kuwa majeruhi, kitu ambacho kitamfanya kutokuwa kwenye uwezekano wa kusajiliwa timu nyingine. Hudson-Odoi amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa za Ujerumani wakati akiwa kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake wa sasa.

Klabu ya Bayern Munich imeripotiwa kutenga kiasi cha pauni milioni 35 kwa ajili ya kumsajili kipindi cha majira ya joto.

Gazeti la Daily Mail limeongeza kwamba Chelsea inaendelea kumshawishi Hudson-Odoi kusaini mkataba mpya mchezaji huyo wa kimataifa wa England.






## *Valverde afunguka moja Barca kutwaa La Liga*

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, ameelezea ushindi wa kikosi chake wa mabao 2-0 dhidi ya Alaves umekuwa na thamani zaidi ya kuelekea kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Carles Alena, ambaye ametokea kwenye akademi ya klabu hiyo, alianza kufunga bao la ufunguzi kwa wageni katika dakika ya tisa kabla ya Luis Suarez kufunga la pili.

Ushindi kwenye dimba la Mendizorroza inamaanisha kwamba Barca wakishinda mchezo mmoja tu watatawazwa kuwa mabingwa wa La Liga katika msimu wake wa saba.

Na Valverde alihamasishwa na ushindi huo na kusema kwamba, kikosi chake kipo kwenye wakati mzuri wa kushinda taji.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, alisema: "Ushindi huu una thamani ya aina yake. Kwa sababu wengi wanaweza kusema kuwa tumeshafikia hatua nzuri kushinda taji, lakini tulitakiwa kufanya hivyo hivyo uwanjani.

"Kuna pointi tatu muhimu zaidi kwa sababu tunajua kuna pointi zaidi na tuna mechi nne mbele yetu."

Ushindi dhidi ya Levante maana yake utawafanya 'La Blaugrana' hao kutangazwa kuwa mabingwa katika mchezo wake utakaopigwa katika dimba la Camp Nou.

## HABARI MICHEZO

# Maurizio Sarri ashtakiwa FA

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, ameshitakiwa na FA kwa utovu wa nidhamu aliouonyesha wakati timu yake ikitoka sare ya kufungana mabao 2-2 na Burnley.

Kocha huyo raia wa Italia alionekana kumvamia kocha mwenzake, Sean Dyche kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Stamford Bridge, na kusababisha kocha msaidizi, Gianfranco Zola kumuomba radhi Dyche kipindi cha pili.

Hata hivyo, mambo yalionekana kuwa ovyo zaidi kipindi cha pili wakati Sarri kwa mara nyingine tena alipovamia kwenye benchi la Burnley.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 60, ameshitakiwa kwa tabia hiyo na sasa anakabiliwa na adhabu.

Katika taarifa yake Chama cha Soka cha England kilisema: "Maurizio Sarri ameshitakiwa kwa utovu wa nidhamu aliouonyesha wakati Chelsea ikicheza na Burnley.

Baada ya mchezo huo, Sarri alikataa kuzungumza lolote na vyombo vya habari na badala yake msaidizi wake Zola ndiye aliyechukua jukumu hilo.





# POCHETTINO: ERIKSEN ATABAKIA SANA SPURS

**LONDON,** England

MAURICIO Mauricio Pochettino, amebainisha kwamba ana matumaini, Christian Eriksen atasaini mkataba mpya na kuendelea kubaki hapo Tottenham baada ya raia huyo wa Denmark kufunga bao la ushindi la dakika za mwisho dhidi ya Brighton Jumanne.

Bao hilo la mchezaji huyo wa zamani wa Ajax, liliwasaidia miamba hao wa London Kaskazini kuendelea kung'ang'ania nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, huku zikiwa zimebakia mechi tatu kufikia tamati.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, mkataba wake wa sasa hapo Spurs unamalizika mwaka 2020, na uvumi umeenea kwamba kiungo huyo majaliwa yake ya baadaye yapo shakani.

Lakini akizungumza mara baada ya mchezo huo wa ushindi, Pochettino alibainisha kwamba: "Ni hali ambayo ipo sawa, Christian Eriksen ni mtu wa aina yake, nafikiri sisi wote ni wa aina yake, tofauti na tunahitaji kuelewa hilo.

"Muda wa yeye kukubaliana na klabu au mchezaji yeyote inategemea na wakati ambao tutaona kuwa muafaka kwa mchezaji.

"Natumaini Christian anaweza kuwa na sisi kwa siku za usoni, lakini nafikiri Christian na sisi tupo wazi kabisa na tutaangalia nini kitatokea."

Aliongeza: "Nafikiri tunakaribia kufikia mwisho wa msimu, ni muda wa mwisho wa kuzungumza na nafikiri jambo la muhimu ni sasa na si kwa yeye peke yake."

# Supercopa ya Hispania kupigwa Saudi Arabia

**MADRID,** Hispania

SHIRIKISHO la Soka la Hispania (RFEF), linakaribia kusaini mkataba ambao unaifanya michuano ya Supercopa kufanyika nchini Saudi Arabia kuanzia mwaka 2020 kwa kipindi cha miaka sita.

Kombe la Supercopa ambalo linafanana na lile la Ngao ya Jamii la Ligi Kuu ya England, huwa linamkutanisha mshindi wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga na bingwa wa Copa del Rey, ikiwa pia ni ishara ya kufunguliwa pazia la Ligi Kuu.

Kati ya mwaka 1982 na 2017 zilikuwa zinacheza mechi mbili, lakini kuanzia mwaka huu imebadilishwa na kuchezwa mchezo mmoja, ambapo Barcelona waliwafunga Sevilla kwenye dimba la Grand Stade de Tanger nchini Morocco.


Lakini Supercopa sasa inaweza kuchezwa nje ya Hispania kwa mujibu wa Gazeti la Marca, huku RFEF ikiwa kwenye mazungumzo na serikali ya Saudi Arabia ambapo sasa kombe hilo litachezea Mashariki ya kati hadi mwaka 2026.

Imedaiwa kwamba, mpango huo, ambao utathibitishwa zaidi baadaye mwezi huu utaanza rasmi mwakani kwa thamani ya euro milioni 30 kwa msimu.

Mazungumzo kati ya pande hizo mbili bado hayajafikia makubaliano ya mwisho, na Gazeti la Marca limeongeza kwamba Shirikisho la Soka la Ufaransa linaamini litafikia makubaliano.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA A
# MAGAZETI YA YA



# STERLING AMTOSA VAN DIJK AMPA KURA KANE

## ●●● Kumekuwa na mengi yanazungumzwa kuhusu Va Dijk, nilijua atakuwa na kura...

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester City, Raheem Sterling, ameweka wazi kuwa amempigia kura mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Kulipwa wa Mwaka England (PFA), na si beki wa Liverpool, Virgil van Dijk.

**Sterling na Van Dijk ndiyo wanaongoza katika mbio hizo za PFA zitakazohitimishwa katika sherehe maalum Jumapili jijini London.**

Van Dijk alisema amempigia kura Sterling - ambaye amefunga mabao 17 kwenye Ligi Kuu England, EPL na kutoa pasi za mwisho ['assists'] tisa msimu huu kwa mabingwa hao watetezi wa EPL.

Hata hivyo, Sterling hakurejesha wema huo, na badala yake akaamua kumchagua mchezaji mwenza wa timu ya Taifa ya England, Kane, ambaye hakupenya katika sita bora ya orodha hiyo.

"Ni vizuri kutambulika mbele, lakini kwa kuwa mkweli, kama hukutwaa EPL, ukweli sitaki kuwa katika mjadala huo," alisema Sterling.

"Ninachotaka kukifanya ni kutwaa ubingwa wa EPL, kutwaa ubingwa wa Kombe la FA, na kisha kufikiri vitu kama hivyo, ingawa tuzo hiyo ni kabla ya hilo. Bila hilo, kweli haileti maana kwangu.

"Nimempigia kura Harry Kane. Kura yangu kwake ni kwa sababu amefunga mabao mengi kila mwaka, amefanya mengi kwa timu, kuisaidia mengi timu.

"Kumekuwa na mengi yanazungumzwa kuhusu Virgil van Dijk. Nilijua atakuwa na kura nyingi, hivyo nikatazama mtu fulani niliyedhani atakuwa karibu yake katika timu ya taifa, jinsi anavyoiweka kazi yake, maadili ya kazi, jinsi anavyojiangalia.

"Mara zote yupo pale, zaidi akitokea katika kuuguza majeraha, kama mtaalamu nilimtazama yeye na hiyo ndiyo sababu ya kumpigia kura, kumuona siku hadi siku katika timu ya taifa."

Mchezaji mwenza wa Sterling katika kikosi cha Man City, Sergio Aguero na Bernardo Silva pia wapo katika mbio hizo za kutwaa tuzo hiyo, pamoja na mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane na kiungo wa Chelsea, Eden Hazard.

## ZISIKUPITE

### RC7 AWAVUTA ISCO, VARANE

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo, anaitaka klabu yake kuwasajili wachezaji wawili kutoka Real Madrid, Isco, 27, na beki wa kimataifa wa Ufaransa, Raphael Varane, 25, majira haya ya joto. ***(Corriere dello Sport)***

### FIFA KUAMUA COUNTIHO

MAJALIWA ya baadaye ya kiungo mshambuliaji wa Barcelona, Philippe Coutinho, mwenye umri wa miaka 26, yatategemea ikiwa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), litaamua kuchelewesha marufuku ya kusajili kwa klabu ya Chelsea ambayo inamtaka, huku Manchester United pia wakimfuatilia kwa karibu mchezaji huyo raia wa Brazil . ***(The Mirror)***

### DAU LA ZAHA KIKWAZO UEFA

KLABU ya Crystal Palace imetakiwa kushusha dau lao la pauni milioni 75 wanalotaka ili kumtoa Wilfried Zaha, 26, ikiwa mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast anataka kuhamia katika timu inayoshriki Ligi ya Mabingwa Ulaya. Tottenham, Arsenal na Manchester United wote wanamuwania. ***(Star)***

### YAHOFIA KUMPOTEZA SANE

MANCHESTER City wanahofu kuwa winga wao, Mjerumani Leroy Sane, 23, anaangalia uwezekano wa kuondoka kwenye klabu hiyo kutokana na kwamba mazungumzo ya mkataba wake mpya yamekwama. ***(Metro)***

### TRIPPIER, WAN-BISSAKA LULU

MANCHESTER United imepanga kumsajili beki wa timu ya Taifa ya England anayekipiga Tottenham Hotspurs, Kieran Trippier, kama wakishindwa kumshawishi Aaron Wan-Bissaka, kutoka Crystal Palace. ***(Mirror)***

### MEUNIER ASHUKA BEI SOKONI

BEKI wa kulia wa Klabu ya Paris Saint-Germain, Thomas Meunier, 27, raia wa Ubelgiji anatajwa kwamba anaweza kununuliwa kwa bei nafuu zaidi na Manchester United kama wakimhitaji. ***(Independent)***

### GATTUSO KUMRITHI BENITEZ

NEWCASTLE wanaangalia uwezekano wa kumchukua kocha wa AC Milan, Gennaro Gattuso raia wa Italia mwenye umri wa miaka 41, ili kurithi mikoba ya Rafael Benitez, 59, ikiwa ataamua kuondoka mwishoni mwa msimu huu. ***(Gazzetta)***

### BENCHI KUMWONDOA MAHREZ

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Riyad Mahrez, 28, anatishia kuondoka kwenye klabu hiyo na winga huyo raia wa Algeria amekwishalalamika wazi juu ya kunyimwa muda wa kucheza chini ya kocha Pep Guardiola. ***(Daily Mail)***

### FELIX AWINDWA JUVENTUS

KIUNGO wa Klabu ya Benfica, Joao Felix, raia wa Ureno anaongoza kwenye orodha iliyotolewa na mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo, 34, katika wachezaji wanaowaniwa na klabu yake. ***(Corriere dello Sport)***

### OBLAK KUMRITHI DE GEA

GOLKIPA namba moja wa Atletico Madrid, Jan Oblak, 29, raia wa Slovenia ni kipa namba moja katika orodha ya Manchester United ya walinda mlango wanaoweza kurithi mikoba ya David de Gea, wakati hatma ya raia huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 28 pale Old Trafford ikiwa haieleweki. ***(Metro)***

## HABARI MICHEZO

# OKWI, NIYONZIMA WATOA NENO UBINGWA

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

WACHEZAJI nyota wa Simba, Mganda Emmanuel Okwi na Haruna 'Fabregas' Niyonzima, wamesema licha ya kukabiliwa na changamoto ya ratiba, nia na malengo yao ni kuhakikisha wanatetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao wanaushikilia.

Niyonzima alifunga bao la kwanza na Okwi ambaye juzi alifikisha mabao tisa, alipachika wavuni goli la pili na kuipa Simba ushindi wa 2-0 dhidi ya Alliance FC katika mchezo wa ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

**Wakizungumza na Nipashe jijini hapa, wachezaji hao walisema mipango yao ni kucheza kwa bidii ili kushinda taji hilo kwa sababu wanahitaji kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika hapo mwakani.**

Okwi alisema kila mchezaji anayepata nafasi ya kucheza katika mechi hizo zilizosalia, huwa anawaza kuisaidia timu kuondoka na pointi tatu na si jambo lingine.

"Tunajua sio kazi rahisi, lakini ni lazima tuhakikishe tunatetea ubingwa wa ligi, hii ndio nafasi pekee tuliyonayo, tunajipanga kuhakikisha tunatimiza malengo yetu," alisema mshambuliaji huyo.

Naye Niyonzima alisema mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo bado ni ngumu, lakini endapo watashinda mechi mbili zilizobaki katika mikoa ya Kanda ya Ziwa watakuwa wamejiweka katika mazingira mazuri.

"Malengo yetu ni kutetea ubingwa tu, tunajua tunakabiliwa na ushindani, pia tunaelewa si kazi rahisi kufikia malengo haya, ila tutapambana kuhakikisha tunashinda kila mechi iliyoko mbele yetu," alisema kiungo huyo wa zamani wa APR ya Rwanda na Yanga ya Tanzania. Aliongeza kuwa uamuzi wa kutoa nafasi kwa kila mchezaji kucheza mechi hizo za ligi ambazo zimepangwa kwa tofauti ya siku moja au mbili, unalenga kupata matokeo mazuri na hiyo ndio tafsiri sahihi ya kikosi kipana.

"Tunaomba mashabiki wetu waendelee kuwa pamoja nasi ili tuweze kuwapa furaha," Niyonzima alisema. Mabingwa hao watetezi leo wanashuka kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa ili kuwakabili KMC FC ya Dar es Salaam ambayo nayo ililichagua dimba hili baada ya Uwanja wa Taifa kutumika kwa michuano ya Vijana wa umri chini ya miaka 17 ya Afrika ( Afcon U-17).

## Mamilionea ya SportPesa yatua Biharamulo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Jackpot ya SportPesa kwa sasa imefika Sh. milioni 624.2 ambazo unaweza kushinda kutumia Sh. 2,000 tu endapo kama utapatia ubashiri wako wa mechi zote 13 kwa usahihi, bado mamilioni ya shilingi yameendelea kutolewa kupitia bonasi kwa wanaopatia mechi 10, 11 na 12 kila wiki.

Na kwa wiki hii imeanza vizuri kwa bahati kumwangukia Ibrahim Lucumay, mkazi wa Biharamulo baada ya kubashiri na kupatia mechi 12 kati ya 13 na kujinyakulia bonasi ya Sh. milioni 43.

"Nilivutiwa sana kucheza na SportPesa ni malipo ya papo hapo. Siku moja nilicheza 'multibet' kwenye Kampuni ya SportPesa na kampuni nyingine ya kubashiri, SportPesa walinilipa baada ya mechi ya mwisho kuisha na kampuni nyingine walinilipa baada ya siku mbili. Kutoka hapo sikuwahi tena kucheza na kampuni nyingine ambayo tofauti na SportPesa.

"Pia kilichonifanya niendelee kucheza na SportPesa ni baada ya kuona Jackpot imefikia milioni 200 ambayo haipo kwenye kampuni yoyote.




Meneja wa Bia ya Castle Lager, Pamela Kikuli (kulia), Balozi wa Castle Africa 5s Tanzania, Ivo Mapunda (katikati) na Meneja Udhamini wa Tbl, David Tarimo, wakionyesha zawadi za washindi wa fainali za Castle Africa 5s zinazotarajiwa kufanyika Jumamosi katika Viwanja vya Posta jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas, akimkabidhi mfano wa hundi Ibrahim Lucumay, baada ya kupatia mechi 12 kati ya 13. **PICHA: SPORTPESA**

## *Timu 32 zitakazovaana Castle Lager Africa 5s hizi*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL), kupitia Bia yake ya Castle Lager, imetangaza timu 32 zitakazoshiriki mashindano ya Soka ya Wanaume ya Castle Africa 5 – Aside [wachezaji watano kila upande] Jumamosi yatakayofanyika katika Viwanja vya Posta Kijitonyama jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa Bia ya Castle Lager Pamela Kikuli, alisema fainali za mashindano hayo zitakazoshirikisha timu 32, zote zinatoka katika vitongoji mbalimbali vya jijini Dar es Salaam na kwamba anatarajia kuona ushindani mkali kutokana na namna timu zilivyojiandaa.

Alisema mashindano hayo ambayo yanafanyika hapa nchini kwa mara ya pili, yamekuwa yakifanyika katika nchi nyingine za Afrika ambapo, mwaka jana Tanzania ilishiriki katika mashindano hayo katika kiwango cha kimataifa nchini Zambia kwa upande wa wanaume.

"Mwaka jana tuliyafanya kwa mara ya kwanza na kupata mwakilishi aliyeshiriki katika michuano ya Kimataifa ya Afrika, huko Zambia kwa kuzikutanisha timu za Afrika ya Kusini, Zimbabwe, Swaziland Lesotho na wenyeji Zambia.

"Lengo ni kuwafikia wanywaji wa bia ya Castle Lager ikiwa ni pamoja na kuwapa fursa ya kutimiza ndoto zao," alisisitiza.

Kikuli pia alisema fainali hizi zitasindikizwa na burudani ya muziki kutoka kwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya ambao ni Mr. Blue na Mauwa Sama, lakini pia patakuwa na Dj Kwame sambamba na mpiga drum wake.

Naye Meneja Udhamini wa Tbl, David Tarimo, alizitaja zawadi za washindi kuwa kwa bingwa mbali na kombe na medali za dhahabu atazawadiwa Sh. milioni 1.5 huku mshindi wa pili akiibuka na medali za shaba na Sh. 900,000 wakati mshindi wa tatu akiibuka na medali za fedha na Sh. 600,000.

Kwa upande wake Balozi wa Bia ya Castle Lager, Ivo Mapunda alizitaja timu zitakazoshiriki fainali hizo mwaka huu kuwa ni Four Ways Park ya Kinondoni, Terminal Villa ya Mbezi Mwisho, STK Pub (Tabata), Namanga Park (Tegeta), Jacks Pub (Makumbusho), KB Bar (Tegeta), Honey Pot (Sinza), Mivumoni Resort (Tegeta), Maduka Matatu (Mwananyamala), Kisuma Bar (Mbagala) na Korner (Sinza), Maseo Bar (Mkwajuni), Mikumi Bar (Mbagala), Mikasa Bar (Ubungo) na Pade Mapambano ya Buza. Nyingine alizitaja kuwa ni Masai Club (Kinondoni), Jambo Lee (Kawe), News Sinza Uzuri (Sinza), Valabendah (Pugu), Ukonga Recreation (Ukonga), Texas Bar (Goba), Anex Bar (Salasala), Benny Pub (Buguruni), Shirima Bar (Ubungo), Safari Pub (Gongo la Mboto), Doctor's Park (Kibamba), Sonata Pub (Chanika), Uhuru Park (Buguruni), Kilwa Road Bar (Temeke), Soccer City (Sinza), Meeda Bar (Sinza), Panama Bar (Kibamba), Rungwe Bar (Tabata), Pentagoni Bar (Kitunda) na Green Palm (Kunduchi).

# Michezo

Alhamisi Aprili 25, 2019

Nipashe




Sterling amtosa Van Dijk ampa kura Kane HABARI UK. 30



Dele Alli akijaribu kuifungia Spurs huku mabeki wa Brighton & Hove Albion na kipa wao wakiwa makini kuokoa, katika mechi hiyo ya Ligi Kuu England iliyopigwa kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur na wenyeji kushinda 1-0 kwa bao la usiku (dk. 88) lililozamishwa nyavuni na Christian Eriksen. **HABARI UK. 29**

# Aussems aiandalia KMC kikosi tofauti

## ●●● Atoa sababu ya mabadiliko, ufundi, uzoefu kutawala leo Kirumba huku akieleza...

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

UFUNDI, uzoefu na ushindani ni vitu vinavyotarajiwa kuonekana katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya wenyeji KMC FC dhidi ya Simba itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa.

**Akizungumza na Nipashe jijini hapa jana, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, alisema anahitaji kupata ushindi katika mchezo huu wa leo ili aendelee kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutetea ubingwa wa ligi ambao wanaushikilia na kwamba mabadiliko ya kikosi yataendelea kufanyika kila mechi.**

Aussems alisema anajua kila mechi wanayocheza ni sawa na fainali, lakini wamejipanga kuwakabili kiufundi zaidi KMC ambao wataingia uwanjani wakiwa wamepata muda mrefu wa kujiandaa na mchezo huo wa raundi ya 26.

Mbelgiji huyo alisema wachezaji wake watacheza kwa nidhamu kwa sababu anaifahamu KMC inaundwa na kikosi chenye wachezaji chipukizi na wazoefu, ambao wakati wowote wanaweza kubadilisha matokeo.

"Tulipoteza mechi dhidi ya Kagera Sugar, kilichobakia tunahitaji kushinda katika mchezo wa Alhamisi (leo) na Jumamosi (dhidi ya Biashara United) ili kupata pointi tisa ambazo zitatuweka katika nafasi nzuri zaidi ya kutwaa ubingwa, ila mechi zote tunahitaji kucheza kwa kiwango cha juu, " alisema Aussems.

Kocha huyo aliongeza kuwa ili kupata matokeo mazuri, ataendelea kufanya mabadiliko katika kikosi chake na uamuzi huo ni maalumu kwa kuwapumzisha nyota wake na vile vile unatoa nafasi kwa kila mchezaji aliyesajiliwa Simba kucheza.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kila mechi kwao ni muhimu na wamejipanga kutorudia makosa yaliyojitokeza mkoani Kagera kwa kuruhusu kufungwa.

"Huu muda ni wa majeruhi, ukipoteza pointi unawaachia wenzako nafasi ya kukaa mahali pazuri, vita bado ni kubwa na hakuna ambaye anahitaji kupoteza pointi tukielekea kumaliza msimu," Rweyemamu alisema.

Etienne Ndayiragije, Kocha Mkuu wa KMC FC, alisema kuwa timu yake imefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kuwakabili mabingwa hao watetezi ambao wamekuwa katika kiwango kizuri zaidi msimu huu.

"Tuko tayari na tunawasubiri kukutana nao, kama wachezaji wangu watafuata vema maelekezo niliyokuwa nawapatia, ninaamini tutashinda mechi hii, tunahitaji pointi tatu muhimu na hatutarajii kutumia uchovu walionao kuwadharau," Ndayiragije alisema.

Simba bado wako katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 63 wakati KMC yenye pointi 42 iko katika nafasi ya saba.

## Barca yataja ya ubingwa La Liga

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, ameelezea ushindi wa kikosi chake wa mabao...




HABARI UK 28

## Hudson-Odoi avuta pumzi

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI kinda wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, amekataa kufanya maamuzi kuhusu majaliwa yake ya baadaye...



HABARI UK 28

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >